# Nipashe

Jumamosi Desemba 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580113

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

UNDER THE SAME SUN ARIGATOU INTERNATIONAL GNRC CEFA




## Daktari kortini tuhuma utoaji mimba, uhujumu

UKURASA 2

# JPM apigilia msumari laini za simu kuzimwa

• **Aongeza** siku 20 usajili alama za vidole, asema hakuna msalie mtume siku ikifika...*Endelea ukurasa 2*




Rais John Magufuli akifanya usajili wa alama ya vidole wakati alipotembelea duka la Airtel Money mjini Chato, mkoani Geita jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Chanzo kifo bosi Zam Zam chatajwa

UKURASA 3

RIPOTI MAALUMU

## Mitego ya wahadhiri kwa wanafunzi rushwa ngono

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


**MICHEZO** **SIMBA SC, KMC FC MAJARIBUNI BARA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## NIDA: Wananchi hawana taarifa usajili kwa vidole

**Na Maulid Mmbaga**

ZIKIWA zimebaki siku 23 kabla ya kufungwa kwa usajili wa alama za vidole, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imebaini wananchi wengi hawana taarifa za kutosha kuhusu usajili huo.

Usajili huo ulitarajiwa kufungwa Desemba 31, mwaka huu, lakini jana Rais John Magufuli alitangaza kuongeza siku 20 hadi Januari 20, mwakani kwa wananchi ambayo watakuwa hawajakamilisha usajili kwa alama za vidole kufikia tarehe ya mwisho iliyotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

Akizungumza na Nipashe jana Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam ambako NIDA imeweka kituo mahsusi kwa ajili ya kuhudumia wananchi wanaohitaji vitambulisho ili kukamilisha usajili huo, msemaji wa mamlaka hiyo, Thomas William, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa wananchi kusaka vitambusho hivyo.

Hata hivyo, William alisema wamebaini wananchi wengi hawana taarifa za kutosha kuhusu usajili huo na wengi wanafika kusaka kitambulisho cha taifa bila kuwa na taarifa za msingi zinazohitajika.

Alisema awali katika kituo hicho walikuwa wanatoa huduma kwa watu 50 kwa siku, lakini katika kipindi hiki cha mwishoni mwa mwaka na ambacho tarehe ya kuzimwa kwa laini za simu zisizosajiliwa imekaribia, wanatoa huduma kwa wateja zaidi ya 1,000 ndani ya saa 10 kila siku.

"Pamoja na kuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi katika zoezi hili, wengi wao hawana taarifa za kutosha zinazowawezesha kupatiwa huduma kwa ukamilifu," alisema.

Aliongeza kwamba namba na vitambulisho zinatolewa kwa wananchi waliokamilisha usajili, lakini kuna baadhi yao wanahitaji kupatiwa vitambulisho kabla hawajakamilisha taarifa zao, kitu ambacho hakiwezekani.

Alisema mamlaka inajitahidi kufanya kazi hadi siku za mwishoni mwa wiki na za sikukuu ili kuhakikisha kila mwananchi anapata kitambulisho, kitachomwezesha kusajili laini yake ya simu kwa alama za vidole.

"NIDA imetoa namba zaidi ya milioni 17, ila kuna watu takriban milioni saba wenye laini za simu na vitambulisho, lakini vinaonyesha havijatumika katika usajili wa alama za vidole," alibainisha.

Muhamed Suddy, mwananchi aliyekutwa na Nipashe jana Mnazi Mmoja akifuatilia mchakato wa usajili huo, alilalamikia uongozi wa NIDA, akidai baadhi ya watendaji wake hawatoi maelezo ya kina kwa wananchi.

"Baadhi ya watoa huduma wa NIDA hawatoi maelekezo ya kijitosheleza, hivyo uongozi ujitahidi kutoa elimu elekezi kwa wananchi jinsi gani ya kujaza taarifa kwenye fomu za usajili," alishauri.

# JPM apigilia msumari laini za simu kuzimwa

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli ameongeza siku 20 kwa wananchi ambao watashindwa kusajili laini zao kwa alama za vidole kufikia Desemba 31 ambayo ilikuwa siku ya mwisho ya usajili wa mfumo huo.

Muda ulioongezwa na mkuu huyo wa nchi utaanzia Januari Mosi hadi Januari 20 mwakani.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilieleza kuwa Rais Magufuli ameongeza muda huo, ili kuwapa nafasi ya kujisajili wananchi ambao watashindwa kukamilisha utaratibu huo katika kipindi cha kuishi Desemba 31 mwaka huu kilichotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, jana Rais Magufuli alisajili laini yake ya simu kwa alama za vidole mjini Chato mkoani Geita na kuwasisitiza Watanzania wote wahakikishe laini zao za simu zinasajiliwa kwa utaratibu huo ulioelekezwa na TCRA.

"Rais Magufuli ameongeza siku 20 kuanzia Januari Mosi hadi 20 kwa wote ambao watashindwa kusajili laini zao katika kipindi cha kuishia Desemba 31, 2019 kama ilivyotangazwa na TCRA kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo kuugua na kukamilisha upataji wa namba ama vitambulisho vya taifa," ilielezwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.

Katika taarifa hiyo, ilielezwa zaidi kuwa Rais Magufuli amesisitiza kuwa baada ya muda huo, hakuna kisingizio chochote kitakachokubalika na ameagiza TCRA kuhakikisha laini ambazo hazijasajiliwa zinazimwa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Magufuli amesisitiza usajili wa laini za simu kwa alama za vidole ni muhimu kwa usalama wa nchi ikiwamo kuepusha vitendo vya utapeli na ujambazi vinavyofanywa na wahalifu, ambao licha ya wengi wao kukamatwa na vyombo vya dola, wameendelea kusababisha usumbufu na upotevu wa mali za wananchi hususani fedha.

Baada ya kusajili laini yake ya simu, Rais Magufuli aliwasalimu wananchi wa Chato mjini waliojitokeza kushuhudia wakati akisajili na kusikiliza maoni yao kuhusu usajili huo.

Steven Wandwi, mfanyabiashara wa chipsi na mishikaki, aliwaongoza wananchi wenzake kumwombea Rais Magufuli na kumshukuru kwa utumishi wake mzuri ulioongeza kasi ya maendeleo kwa taifa hasa vijana, ambao sasa wanachapa kazi bila bughudha.

Kabla ya kwenda kusajili laini yake ya simu, Rais Magufuli alitembelea Mtaa wa Chato Kati na kutoa pole kwa familia ya Athanas Mnaku, aliyefariki dunia Desemba 25, mwaka huu.



Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakiwa kwenye foleni nje ya Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kwa ajili ya kupata vitambulisho hivyo, huku zikiwa zimebakia siku chache ambapo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuzima laini za simu ambazo hazijasajiliwa ifikapo Januari 20, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Daktari, muuguzi kizimbani tuhuma utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

DAKTARI wa Hospitali ya Dental Clinic, Awadhi Juma (40) na mwenzake, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo na ya utoaji wa mimba.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni muuguzi wa hospitali hiyo, Kidawa Ramadhani (26). Washtakiwa hao kwa pamoja walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, akisaidiana na Wakili wa Serikali Glory Mwenda, kwa nyakati tofauti waliwasomea washtakiwa hao mashtaka yao.

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa Oktoba, mwaka huu, eneo la Sinza Mori, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wakiwa na lengo la kutoa mimba, waliingiza bomba la sindano katika sehemu za siri za wanawake wawili tofauti (majina yamehifadhiwa) na kusababisha kuharibika kwa mimba zao.

Ilidaiwa kuwa Agosti, 2002 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Juma kwa lengo la kudanganya, alighushi cheti cha Diploma cha Utaalamu wa Tiba ya Kinywa akionyesha ni halali kimetolewa na Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa Juma pia anadaiwa kwamba Februari 20, 2015 jijini Dar es Salaam, alighushi leseni ya biashara ya tarehe hiyo akionesha imetolewa na Manispaa ya Kinondoni wakati akijua si kweli.

Ilidaiwa kwamba kati ya Mei, 2015 hadi Desemba 4, mwaka huu, mshtakiwa huyo alikutwa akimiliki hospitali ya tiba ya meno bila kibali.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo kwa nia ya kudanganya, alijiita daktari kinyume cha sheria huku akijua si kweli.

Katika shtaka jingine ilidaiwa kuwa katika tarehe za tukio la sita, Juma alitakatisha na kujipatia Sh. 260,000 wakati akijua fedha hizo ni zao la kosa la jinai la kughushi.

Upande wa Jamhuri ulidai, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Januari 10, 2020 kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa walirudishwa rumande kwa kuwa mashtaka ya kutakatisha fedha hayana dhamana.

## HABARI KITAIFA



.Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, akisalimiana na Mbunge wa Jimbo la Lulindi, Jerome Bwanausi, wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ukumbi wa William Matwani Hall, ambaye ni baba mzazi wa Mkapa katika Parokia ya Nanjota Jimbo la Tunduru-Masasi jana, wilayani Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Polisi wataja chanzo kifo Mkurugenzi wa Zam Zam

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BAADA ya kudaiwa kuwapo kwa utata kuhusu kifo cha Mkurugenzi wa Taasisi ya The Dalai Islamic Centre na Mmiliki wa Shule ya Zam Zam, Rashid Bura (62), Jeshi la Polisi limeeleza chanzo chake.

Jeshi hilo limedai Bura alifariki dunia kutokana na matatizo ya moyo baada ya kuibuka maswali mengi kuhusu kifo hicho, ikidaiwa mwili ulikutwa ofisini kwake ukiwa hauna nguo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alidai jana kuwa katika uchunguzi wa awali na ripoti ya daktari, imebainika kuwa kifo cha marehemu Bura kilitokana na ugonjwa wa moyo.

Alidai kuwa Bura, ambaye ni mkazi wa Chang'ombe Extension jijini, alipatwa na umauti akiwa ofisini kwake baada ya safari ya kutokea Dar es Salaam.

"Desemba 21, mwaka huu, Bura alihudhuria mkutano wa uhusiano wa dini mbalimbali huko jijini Dar es Salaam na kurejea jijini Dodoma Desemba 22, mwaka huu," alidai.

Alidai kuwa baada ya kurejea jijini Dodoma, Bura alienda ofisini kwake Mtaa wa Nyerere, Kata ya Madukani na akiwa ofisini, alipatwa na tatizo la moyo lililosababisha kifo chake.

Kamanda Muroto aliongeza kuwa kabla ya kugundulika kuwa amefariki dunia akiwa ofisini, Bura alikuwa amepoteza mawasiliano na familia yake baada ya simu yake kuzima.

Inadaiwa kuwa Desemba 25, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni, mtoto wake, Ally Mussa, alikwenda ofisini kwake na kukuta amefariki dunia na mwili wake ukiwa umeharibika.

"Jeshi la Polisi lilifika eneo la tukio na wataalamu wa uchunguzi wa matukio kuchunguza tukio hilo, eneo la tukio ulifanyika uchunguzi na

INAENDELEA UK. 8

# Japan yatoa bil. 4.2/- kufufua Tafico

**Na Peter Haule**

TANZANIA imepokea msaada wa Yen za Japan milioni 200 (Sh. bilioni 4.2) kutoka serikali ya Japan kwa ajili ya kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (Tafico).

Mkataba wa msaada huo ulitiwa saini jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, kwa niaba ya serikali ya Tanzania na Naibu na Kaimu Balozi wa Japan nchini, Katsutoshi Takeda, kwa niaba ya Japan.

James alisema kuwa msaada huo utatumika kununua meli ya uvuvi yenye vifaa vya kisasa, mashine ya kutengeneza barafu, ghala la baridi la kuhifadhia samaki, vifaa mbalimbali vya kuvulia samaki na vya karakana, gari lenye mitambo maalum ya barafu na gari kwa ajili ya kusambazia samaki.

Alisema utekelezaji wa mradi huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili (FYDP II), ambayo pamoja na mengine, unalenga kuboresha uvuvi na hatimaye kuvutia Watanzania zaidi kujihusisha katika sekta hiyo kama shughuli kuu ya kujipatia kipato.

"Mradi huu utaongeza uuzaji wa samaki nje ya nchi, kuongeza uhakika wa chakula nchini na pia utaboresha usindikaji wa samaki, kuongeza thamani na masoko na kupunguza upotevu wa mazao ya samaki baada ya kuvua," alisema James.

Alisema kiwango cha ukuaji kwa shughuli ndogo za kiuchumi za uvuvi kilifikia asilimia 9.2 mwaka jana ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.4 mwaka 2017, huku akibainisha kuwa kilitokana na utunzaji mzuri wa mazalia ya samaki yakiwamo mabwawa ya watu binafsi sambamba na kuongezeka kwa mahitaji katika soko la ndani na nje.

James alisema shughuli za uvuvi zilichangia asilimia 1.7 katika pato la taifa mwaka jana, hali ambayo inadhihirisha umuhimu wa uvuvi katika uchumi.

Alisema msaada uliotolewa utachangia jitihada za serikali katika kufikia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo Endelevu ya mwaka 2030 na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063.

Serikali ya Japan, alisema imekuwa ikiisaidia Tanzania kupitia misaada na mikopo nafuu katika sekta mbalimbali kama kilimo, miundombinu ya barabara, maji, nishati utawala bora na wwajibikaji na kwamba mpaka sasa jumla ya Sh. trilioni 1. 3 zimetolewa na serikali hiyo tangu mwaka 2012.

Misaada na mikopo hiyo, alisema inadhihirisha kuwa kuna uhusiano mzuri wa kirafiki kati ya Tanzania na Japan, hivyo matumaini ni kuwa urafiki huo utaendelea kuimarishwa na serikali zote mbili kwa ajili ya maendeleo ya nchi hizo.

Kwa upande wake, Takeda, kwa niaba ya serikali ya Japan, alisema nchi yake itaendelea kuisaidia Tanzania kutokana na ushirikiano mzuri kati ya nchi hizo mbili, lakini kuchangia jitihada za Tanzania katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa wananchi wake.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamahtamah, alishukuru serikali ya Japan kwa msaada huo utakaosaidia kufufua shirika hilo.

Alisema serikali itapeleka muswada bungeni Januari, mwakani, ili kuiwezesha Tafico kuanza kazi zake rasmi na kwa kishindo ili kuchangia katika uchumi wa taifa kwa kiwango kikubwa.




RIPOTI MAALUM -2

# Hivi ndivyo ilivyo rushwa ngono wasomi vyuo vikuu

## •Udom wakiri mbele ya JPM

Na Sanula Athanas

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilianika picha pana kuhusu rushwa ya ngono vyuoni na kashfa za kisheria zilizoibuka. Je, wenyeji wa madhila hayo wana yapi kuhusu hilo? Endelea kufuatilia undani wa kilichopo...**



MANTIKI ya mtazamo huo wa rushwa ya ngono kutawala mwenendo wa elimu ya juu, pia imekuwa na ushuhuda katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ushahidi wa wazi ni tukio la Novemba 27 mwaka jana, mhadhiri wake alipoanika hadharani kinachojiri ndani ya chuo.

Mtaaluma wa kike, Dk. Vicensia Shule, kupitia ukurasa wake wa Twitter, alimwomba Rais John Magufuli kuingilia kati suala hilo, ambalo kwa nafsi yake alilitafsiri kuwa 'limekithiri' chuoni hapo.

Dk. Shule (41), anayefundisha katika Kitivo cha Sanaa na Ubunifu cha UDSM, alitaka kutumia bango kuufikisha ujumbe wake kwa Rais siku hiyo ambayo mkuu huyo wa nchi alikuwa na ziara ya kikazi chuoni hapo, lakini akaingiwa na hofu.

Sehemu ya nukuu ya ujumbe wake ilisomeka: "Baba @MagufuliJP (Rais Magufuli) umeingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufungua maktaba ya kisasa. Rushwa ya ngono imekithiri mno UDSM.

"Nilitamani nikupokee kwa bango langu, ila ulinzi wako umenifanya ninyamaze. Nasubiri kusikia kutoka kwako, maana naamini wateule wako ni waadilifu, watakwambia ukweli."

Kwa kurejea makundi mbalimbali yenye maslahi ya elimu, ambayo yako mstari wa mbele katika malalamiko kama ya Dk. Shule, inaelezwa kwamba rushwa hiyo ya ngono, inajumuisha wahadhiri wanaoendesha mabaya hayo dhidi ya wanafunzi.

Vilevile, kuna kashfa ya baadhi ya wanazuoni kuhujumiana wao kwa wao kwa madai ya ngono, pale panapoibuka mahitaji ya kusaidiana na kuhudumiana kikazi kwa mujibu wa taratibu zao za kiutendaji, kitaaluma na kimenejimenti. Kama ilivyokuwa kwa SAUT, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, naye mara moja aliunda kamati kuchunguza ukweli wa suala hilo, huku Takukuru nayo ikibeba jukumu lake kwa suala hilo hilo.

Prof. Anangisye anafafanua hatua waliyofikia akieleza kwamba: "Bado (kamati) inaendelea na uchunguzi, hawajakamilisha. Unajua hili suala ni nyeti, linahitaji uchunguzi wa hali ya juu na hawawezi kuliharakisha, lazima wajiridhishe. Na unapounda kamati, ujue inahitaji uhuru."

Wizara mama ya elimu nayo kwa nafasi yake, kupitia Katibu Mkuu, Dk. Leonard Akwilapo, inasema ilipata taarifa hizo kupitia vyombo vya habari na ikachukua hatua ya awali kuwasiliana na uongozi wa UDSM kupata ufafanuzi wa kina, ingawa inakiri tuhuma hizo ni nzito hasa kwa chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhusiano wa Takukuru, Doreen Kapwani, ofisi yake ilichukua hatua mara moja kuchunguza tuhuma hizo ingawa hakufafanua zaidi.

Jana ilitimu mwaka na mwezi mmoja, tangu mwanazuoni Dk. Shule alipoibua tuhuma hizo dhidi ya mahali anapofanya kazi, lakini hadi sasa kimya kikuu kimetanda kuhusiana na mwenendo wa uchunguzi wa kashfa hiyo.

### UDOM WAKIRI

Novemba 21, mwaka huu, uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) ulikiri mbele ya Rais Magufuli kuwapo kwa dosari ya baadhi ya wanazuoni wake kuomba rushwa ya ngono na nyinginezo kwa wanafunzi wao.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Faustine Bee, alisema ni dosari zilizousukuma uongozi kuunda Kamati ya Maadili, mahsusi kubeba jukumu la kudhibiti unyanyasaji wa kijinsia na kupambana na rushwa ya aina hiyo dhidi ya wanafunzi.

Akizungumza kwenye mahafali ya chuo hicho, Rais Magufuli akiwa mgeni rasmi na mmoja wa watunukiwa, Profesa Bee aliwasilisha malalamiko yake mbele ya mkuu huyo wa nchi kwamba, matendo ya baadhi ya watumishi wa Udom yanayokiuka maadili na sheria, yametia dosari kubwa mazuri waliyoyafanikisha.

Katika maelezo yake, Profesa Bee ambaye ametumikia sekta ya elimu kwa muda mrefu, alirejea uzoefu kwamba dosari hiyo imeenea katika vyuo vingi, akifafanua:

"Wafanyakazi wamekuwa wakiomba rushwa ya ngono au fedha kwa wanafunzi ili kuwafaulisha, hali kadhalika, wapo wanafunzi wanaowalazimisha wafanyakazi kuwapa rushwa ya ngono ili kufaulishwa masomo yao."

Ikirejewa historia yake ya utendaji kabla ya kuteuliwa kuongoza Udom Machi mwaka huu, mwanazuoni huyo wa uchumi alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na kabla ya hapo, alikuwa katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA).

Nini kifanyike? Mkuu huyo wa Udom alisisitiza kwamba suala hilo haikubaliki na Baraza la Chuo tayari limekubaliana kuhakikisha linatokomeza mwenendo huo, kwa kutomvumilia yeyote atakayebainika kukumbatia vitendo hivyo.



Makamu Mkuu wa Udom, Profesa Faustine Bee

"Katika kufanikisha hilo, chuo kimeunda Kamati ya Maadili (Anti-Corruption and Intergrity Commitee) ili kudhibiti tabia na mienendo kama hii.

"(Kamati hii) ilishazinduliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, aliyekuwa ameambatana na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Diwan Athumani.

"Pia wanafunzi wameanzisha klabu ya kukabiliana na mambo haya na tunaipa uzito ili kuwa na 'zero tolerance' (kutovumilia hata kidogo) kwenye hili," alisema.

### KAULI YA TAHLISO

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), George Mnali, anailezea rushwa ya ngono kwa kauli kwamba: "Ni suala ambalo lipo katikati, kwa maana linafahamika au kutofahamika kwa kuwa linafanywa kwa usiri mkubwa".

Anasema hali hiyo inatokana na uhalisia kwamba wahusika wa njama hiyo hukubaliana na mazingira waliyojiwekea, akitoa mfano wa matukio yaliyotokea katika chuo kimoja mkoani Iringa (jina tunalihifadhi).

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kashfa hiyo ilimhusu mwanafunzi wa kike aliyetakiwa urafiki na mhadhiri, lakini mwalimu huyo alipokataliwa na kisha akagundua binti huyo ana rafiki wa kiume, alichukua uamuzi mbaya dhidi ya matokeo yao ya mtihani.

Inaelezwa kwamba, rafiki wa kiume ambaye alihisiwa kuwa ndiyo kikwazo cha mafanikio ya mwalimu kimapenzi, alifelishwa na kufungishwa virago na yule wa kike alifelishwa kwa kiwango cha kutakiwa kurudia mtihani, mwalimu akiamini safari hiyo itampa fursa nzuri.

"Jamaa ilifikia hatua akapata 'disco' (kufukuzwa chuo kutokana na kufeli mtihani) akiwa mwaka wa mwisho. Yaani alikuwa muhula wa mwisho na huyo rafiki (mpenzi) yake akapewa 'supp' (kurudia mtihani) ya somo moja, pia akacheleweshwa kupokewa kwa ripoti ya 'research' (utafiti) yake," anasimulia.

Kiongozi huyo wa TAHLISO anaeleza uhalisia wa maisha ya wanafunzi katika vyuo vikuu, akikiri kuwapo rushwa ya ngono na kwamba ni jambo linalowaweka wanachuo njia panda.

"Wanafunzi wanashindwa kuweka wazi jambo hili, kwa sababu wakati nyumbani wanataka shahada, chuoni mwalimu naye kaishikilia shahada yake mpaka apate timizo la ngono.

"Kwa hiyo, unakuta kuna vitu vinakuwa kwenye 'ubinafsi' mkubwa na hata ukiwauliza, kuna uwezekano mkubwa wasikwambie japo wanaumia.

"Lakini, nimeongea na marais kutoka vyuo vitatu, wanasema kwamba imefikia wakati wao wanajitoa mhanga kwamba mwanafunzi akienda kuripoti kwao, inabidi rais amwagize binti huyo akamwambie mwalimu kuwa yeye ni rafiki wa kimapenzi wa rais wa chuo.

"Inabidi marais watumie mbinu hiyo, ili kumlinda mwanafunzi kwa sababu walimu wanaofanya uchafu huo huwa na kawaida ya kuwaogopa marais wa vyuo, lakini bado kuna rais mmoja alifanya hivyo naye akajikuta analimwa 'supp' na huyo mwalimu.

"Baada ya rais kufuatilia sana jambo hilo, mwalimu akamwambia haikuwa 'supp' bali hakuiona karatasi yake ya mtihani wakati anaweka alama.

"Rais alipofuatilia kwenye bodi ya mitihani, akaambiwa karatasi yake ilikuwapo na aliporejea kwa mwalimu husika, mwalimu huyo akaomba msamaha kwa kumtaka asiende kuripoti kwa mkuu wa chuo," anaeleza.

Anasema hatua iliyofikia, rushwa ya ngono imekuwa suala mtambuka, likiwaumizi wanafunzi wa kike na wa kiume kwa wakati mmoja na hasa wale wenye urafiki wa kimapenzi.

Mtazamo wa kiongozi huyo ni kwamba, hali ilikofikia sasa, inajenga msukumo na haja ya kuwapo mfumo wenye nguvu inayotoa mabadiliko ya haraka dhidi ya kilio hicho, kabla hali haijawa mbaya zaidi.

Anatumia fursa hiyo kuishauri Takukuru kuunda dawati maalum la kupambana na rushwa za ngono kwa wanafunzi. Hatua yenye kuitikia wito huo, imeshaanza kuchukua nafasi chuoni Udom.

***FUATILIA JUMATATU IJAYO NAMNA NYAYO ZA WANAFUNZI ZINAVYOJITOKEZA KATIKA KUUMBA KASHFA HIYO.**

# Kilimo michikichi kuokoa bil. 600/- uagizaji mafuta nje

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeanza mkakati wa kuboresha kilimo cha michikichi mkoani Kigoma kwa kupanda miche milioni 20 katika kipindi cha miaka minne ili kuokoa Sh. bilioni 400 hadi 600 zinazotumika kuagiza mafuta ya kupikia nje ya nchi kila mwaka.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao katika Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, alisema jana kuwa mkakati huo unalenga kuokoa kiasi hicho cha fedha ambacho hutumika kila mwaka kuagiza mafuta.

Alisema mkakati huo ulianza mwaka 2018/19 na ndani ya miaka yake minne utakuwa na lengo la kukuza upatikanaji wa mbegu bora za kisasa kwa ajili ya zao hilo.

"Mkakati huu umeanza 2018/19 na unaendelea ndani ya miaka minne ukiwa na lengo la kukuza upatikanaji wa mbegu za michikichi ili kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kupikia nchini," alisema.

Pia alisema kila mwaka wanatarajia kupanda miche milioni tano, ambayo anaamini itasaidia upatikanaji wa miche kwa wakulima wa zao hilo nchini. Nyasebwa alisema upandaji wa miche hiyo unafanywa kwa ushirikiano na Jeshi la Magereza Kwitanga, Ilagala na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi la Burombola mkoani Kigoma na taasisi mbalimbali zinazojihusha na masuala ya mbegu ili kuhakikisha mkakati huo unafanikiwa.

"Serikali imejipanga kuhakikisha inafanikisha utaratibu huo iliojiwekea wa kufanikisha upatikanaji wa michikichi," alisema Nyasebwa.

Hata hivyo, aliwataka wakulima waandae vitalu kuanza kupokea miche ya michikichi kwa ajili ya kupanda tayari kwa kuanza kutekeleza mkakati huo, huku akisisitiza kuwa Wizara ya Kilimo iko mstari wa mbele kuhakikisha inatekeleza upatikanaji wa mbegu bora na za kisasa.

Alisema hivi sasa suala la upatikanaji wa mbegu bora limekwisha na wakulima wajipange kuhakikisha wanakuwa na vitalu vya kupokea miche hiyo ya kisasa.

Inakadiriwa Tanzania huagiza tani zisizopungua 400,000 za mafuta ya mawese kila mwaka ili kukidhi mahitaji licha ya kuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu za mafuta tofauti.

Tanzania inaagiza mafuta ya mawese kutoka Indonesia ambayo inaongoza kwa uzalishaji ikifuatiwa na Malaysia.

# DC aziona fursa za biashara Mbambabay

**Na Elizabeth Zaya,** NYASA

MKUU wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, amesema maboresho ya Bandari ya Mbambabay yanayofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), yatasaidia kufungua fursa za kibiashara katika eneo hilo na nchi jirani kwa kiwango kikubwa.

Akizungumza na waandishi wa habari waliozuru eneo hilo jana, Chilumba alisema kwa kipindi kirefu wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakikumbana na kikwazo cha usafiri, lakini sasa anaamini maboresho hayo yatakuwa suluhisho.

Alisema maboresho hayo pia yatachagiza kuongezeka kwa shughuli za biashara kati ya Tanzania, Malawi na Msumbiji ambazo zinatumia Ziwa Nyasa.

"Katika Wilaya ya Nyasa, kuna fursa nyingi za kibiashara ikiwamo uvuvi wa samaki na machimbo ya makaa ya mawe, shughuli hizi zote haziwezi kutusaidia kama mazingira ya kibiashara hayajaboreshwa na ndiyo maana tunawashukuru TPA kwa kuliona hili," alisifu.

"Tunaiona Nyasa mpya katika siku za usoni, na tumeona pia meli mpya imetengenezwa ambayo itatatua shida kubwa ya usafiri katika eneo hili, tumeambiwa inaanza safari zake mwezi ujao, wananchi wamefurahi na wanaisubiri kwa hamu.

"Tunamshukuru sana Rais John Magufuli, ametuona kwa jicho la kipekee sisi wananchi wa Nyasa, tulikuwa hatuna hata meli moja katika ziwa hili, lakini tangu aingie madarakani, ametuletea meli tatu, tuna meli mbili za mizigo za Mv Ruvuma na Mv Njombe na mwezi ujao, tunaanza kusafiri kwa Mv Mbeya II, ni jambo la heri sana kwetu."

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abedi Gallus, alisema bandari hiyo ya Mbababay inatarajiwa kuanza kupitisha shehena za makaa ya mawe kuanzia Januari mwakani.

Alisema hiyo ni miongoni mwa fursa zinazotokana na maboresho yanayofanywa na TPA pamoja na ujio wa meli hizo mpya.

Imani Masawe kutoka katika Kampuni ya God Mwanga Gems inayochimba makaa ya mawe kwenye mgodi wa makaa hayo katika Kijiji cha Marini, Kata ya Mtipwili wilayani humo, alisema usafirisha bidhaa hiyo kwa njia ya maji utapunguza muda wa usafirishaji na kupunguza gharama.



Sehemu ya maghala 21 ya kuhifadhia korosho iliyobomoka kuta zake wilayani Tunduru mkoani Ruvuma na kuhatarisha usalama wa korosho za wakulima zilizohifadhiwa katika maeneo hayo, hali inayo tishia kuharibu ubora wa korosho hizo na kusababisha kuuzwa kwa bei ndogo. **PICHA: STEVE CHINDIYE**

# Maghala ya korosho yabomoka Tunduru

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MAGHALA 21 ya kuhifadhia korosho yameripotiwa kubomoka kuta zake, hivyo kuhatarisha usalama wa korosho za wakulima zilizohifadhiwa katika maeneo hayo.

Hali hiyo inaelezwa kutishia kuharibika kwa ubora wa korosho hizo na kusababisha kuuzwa kwa bei ndogo.

Taarifa zinaeleza kuwa maghala hayo ni mali ya vyama 13 kati ya vyama vya msingi vya mazao (Amcos) 37 vilivyopo wilayani hapa.

Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Tunduru (Tamcu), Imani Kalembo, alisema hayo jana katika mahojiano maalumu na kwamba hali hiyo huenda ikaathiri ubora wa korosho za wakulima.

Kalembo alisema kuwa hali hiyo imetokana na kuwapo kwa mrundikano mkubwa wa korosho za wakulima katika maghala hayo kulikotokana na mzabuni wa kusambaza magunia kuchelewesha kuyafikisha kwa wakulima.

Alisema hadi Desemba 21, mwaka huu, Tamcu ilikuwa imepokea magunia 240,000 yenye uwezo wa kuchukua kilo milioni 19.2.

Kwa mujibu wa kalembo, kutokana na uzalishaji mkubwa wa zao hilo katika msimu wa mwaka 2019/20, hadi sasa taarifa zinaeleza kuwapo kwa kilo 5,275,597 za korosho ghafi zilizokusanywa kutoka kwa wakulima zikiwa zimemwagwa katika maghala ya Amcos katika maeneo mbalimbali.

Aidha, katika taarifa hiyo, kalembo alisema sambamba na hali hiyo pia yako maghala 14 yameripotiwa kuwa na nyufa na kufanya jumla ya maghala mabovu kuwa 35.

Kwa mujibu wa meneja huyo, maghala hayo ni mali ya Amcos za Asema, Chichilimbe, Mlimi, Mruji, Mshikamano, Mtetesi, Munjapo, Mtetesi, Namitili, Namiungo Nguvumali, Sama na Tinginya.

Alisema hali hiyo imesababisha vyama vya ushirka vya msingi vya wakulima kutumia gharama kubwa katika kuimarisha ulinzi ili kuhakikisha usalama wa korosho za wakulima.

Alisema ili kudhibiti hali hiyo, tayari ofisi yake imetoa maelekezo kwa viongozi wa vyama vyote vilivyokumbwa na kadhia hiyo kujipanga kufanya ukarabati wa maghala yaliyopata nyufa na kujenga maghala yaliyobomoka.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wachezaji dirisha dogo usifanyike kishabiki

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara unatarajiwa kukamilika hivi karibuni, tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeshafungua dirisha dogo la usajili wa wachezaji wapya wanaotarajiwa kuongezwa katika ligi hiyo.

Ligi hiyo ndiyo ya juu kwa upande wa Tanzania Bara, na ndiyo inayotoa mwakilishi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo hufanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Licha ya dirisha hili na kipindi hiki cha usajili kuonekana kuwa kidogo, lakini ni muhimu kwa makocha kuongeza umakini kwa sababu ya kuimarisha vikosi vyao.

Ni usajili ambao unatakiwa kufanywa kwa kuzingatia mahitaji halisi na muhimu kwa timu husika ili iweze kutimiza malengo yake.

Wakati baadhi ya timu zikiwa na mechi za viporo mkononi, lakini ni wazi kwamba klabu karibu zote tayari zimeshabaini mapungufu yaliyoko kwenye vikosi vyao, na huu ndio wakati sahihi wa kutibu matatizo hayo, ili kurejea kwenye ushindani wakati wa mzunguko wa pili au lala salama.

Nipashe inawakumbusha viongozi wa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara pamoja na Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Kuu ya Wanawake, kuwaacha makocha wafanye kazi zao kwa weledi, ili mwisho wa msimu, timu hizo ziweze kupata matokeo mazuri.

Hiki ndio kipindi ambacho, maoni na mapendekezo ya makocha yanatakiwa kufuatwa kama sio asilimia 100, basi angalau iwe asilimia 60, na hapo, ndipo mwisho wa msimu mnaweza kuzungumza lugha moja kama sio kufungua mvinyo kwa furaha.

Najua ni ngumu kwa baadhi ya timu, kutekeleza mapendekezo ya makocha wao, kutokana na hali halisi ya kiuchumi, lakini hali hii haitoi baraka au haimaanishi viongozi wachukue jukumu la kusajili wachezaji au kuwaacha baadhi ya nyota kwa matakwa yao binafsi.

Tunawakumbusha kuwa, kama klabu zetu zinataka kweli kushindana na kufanya vema katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho na Kombe la Kagame, usajili wa "mihemuko" au kukomoana hasa kwa vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga, umepitwa na wakati.

Umefika wakati viongozi wa klabu wanatakiwa kuwaamini makocha wao na kutoweka shinikizo la aina yoyote kwenye mchakato huu muhimu, kwa kuamini uzoefu na elimu walizonazo makocha hao, zitafanikisha kufikia malengo ya timu husika.

Endapo timu itashindwa kutumia vema kipindi hiki cha dirisha dogo, hali inaweza kuwa mbaya na ikikumbukwe kwamba, idadi ya timu zitakazoshuka daraja msimu huu zimeongezeka.


Ingawa idadi ya mechi ambazo hazijachezwa ni nyingi, lakini tayari klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara zimeshajigawa katika makundi mawili, zipo zinazowania ubingwa na zile zinazopambana kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Picha hii inatakiwa kutumiwa kigezo cha kila klabu kutumia wakati huu wa dirisha dogo, kufuta makosa yaliyojitokeza na hatimaye kuanza mzunguko wa pili kwa kuwa na vikosi imara ambavyo vitapambana kusaka matokeo chanya.

Ikumbukwe ligi hii ndiyo inayotegemewa kuimarisha na kutoa nyota watakaopeperusha bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika Aprili mwakani.

Ni ukweli usiofichika, mafanikio ambayo tunayaona leo katika timu za Ulaya au za hapa Afrika kama TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), hayatokani na vitendo vya miujiza, ni matunda ya kufanya kazi kwa weledi, bila kusahau uwezo wa kifedha wa klabu ni sihala namba moja ya kufikia malengo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Umbea wa viongozi unaharibu

Na Barnabas Maro

**UMBEA**/umbeya ni tabia ya kutoa habari bila kutumwa au kuulizwa; udaku udakuzi; tabia ya kufuatilia au kusikiliza habari za watu wengine bila kutumwa.

'Uongozi' ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia au kuongoza shughuli; dhamana ya kusimamia jambo kwenye taasisi au penginepo. Hapa nawazungumzia viongozi wa vilabu vya kandanda, hususan Simba na Yanga.

'Vizabizabina' ni watu wanaofitini watu wa pande mbili zinazohasimiana, wenye tabia ya kuchochea uhasama baina ya watu wa pande mbili.

Mambo yanayofanywa na baadhi ya viongozi wa Simba na Yanga ndio yasababishayo mvutano baina ya timu hizo wakati wa usajili wa wachezaji. Mambo ya siri yanayojadiliwa kwenye mikutano ya ndani, huelezwa kwa baadhi ya wanachama na waandishi wa magazeti kwa masharti ya kutotajwa majina yao.

Kama ni lazima kuwekwa hadharani, kuna wasemaji maalumu walioajiriwa kueleza mambo muhimu ya vilabu kama ni lazima. Hao wanaojitia kimbelembele kutoa siri za vilabu ni wambea na wazandiki (watu wasio wakweli, waongo, wanafiki na wadanganyifu.)

Wahenga waliuliza: "Pilipili usiyoila yakuwashiani?" Maana yake pilipili inayomwasha mtu ni ile aliyoila; asiyoila haiwezi kumwasha. Methali hii hutumiwa kumnasihi mtu asiyaingilie mambo yasiyomhusu. Natamani kama wahusika wangesoma makala haya kwa tafakuri (mawazo mazito; taamuli, mazingatio.)

Wahenga walisema "Siri ya mtungi iulize kata" wakiwa na maana mtungi na kata huhusiana sana. Kwa hiyo siri ya mmoja anaifahamu mwenzake. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa tuzitakapo habari zinazomhusu mtu fulani tunapaswa kumuuliza rafiki yake wa karibu sana.

Wakati wa usajili wa wachezaji wa kandanda nchini, kila klabu huwa na wachezaji waliokusudiwa kusajiliwa na timu mbalimbali. Simba na Yanga ndizo hushindana katika usajili, na timu yenye uwezo mkubwa wa hela ndio huwavutia wachezaji.

Ili kufanikisha usajili, viongozi wa vilabu hujadiliana kuhusu wachezaji wanaofaa kusajiliwa. Jambo hili hufanyika kwa siri na baada ya kukamilishwa ndipo hutangazwa rasmi kuwa mchezaji au wachezaji fulani wamesajiliwa na Simba au Yanga.

Sivyo ilivyo kwa Simba na Yanga. Kila moja huweka hadharani majina ya wachezaji wanaokusudiwa kusajiliwa na timu hizo na magazeti huweka hadharani. Siri huwa si siri tena!

Hali kama hii huwapa nafasi wachezaji wanaotakiwa na vilabu hivyo kuchagua penye hela nyingi ingawa wengine hujiunga na klabu wanayoipenda kwa moyo wote. Tumeona na twaendelea kuona jinsi Simba na Yanga zinavyozidiana maarifa na uwezo katika usajili.

Kwa nini? Kwa sababu siri za usajili hutoka nnje mapema na kuunufaisha upande mwingine unaochukua hatua za haraka kuhitimisha usajili wa mchezaji anayetakiwa na upande mwingine.

Ukiangalia idadi ya wachezaji mahiri waliotakiwa na Yanga, sasa wametwaliwa na Simba na ndiwo wanaozitetemesha timu zingine uwanjani ikiwamo Yanga.

Yalisemwa na wahenga kuwa "Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako." Methali hii yatufunza umuhimu wa kutochelewa tuamupo kufanya jambo fulani. Mvutano wa usajili kati ya Simba na Yanga husababishwa na viongozi wasiokuwa na 'vifua' vya kuficha siri zao. Hudhani kufanya hivyo ni 'sifa' kumbe wanajikaanga kwa mafuta yao wenyewe! Huwa najiuliza: mtu anapotarajia kumposa msichana fulani hutangaza hadharani kabla ya kukubaliana naye? Unapotangaza kabla ya kukubaliana hujui kuwa unawazindua wenzako waliokuwa na lengo hilo hilo?

Kwa sababu hiyo wenzako watachukua hatua mujarabu (yenye kufaa kutengenezea jambo au kutatulia tatizo) kumpata msichana huyo na kukuwacha kwenye mzubao (hali ya kuemewa inayopelekea mtu kushindwa kufanya jambo upesi; bumbuazi.)

Kwa upande mwingine wachezaji wanapaswa kuwa makini sana wanaposajiliwa. Wanapaswa kuwa na wanasheria wao watakaowaongoza kabla ya kukubaliana na kusaini mikataba na vilabu vinavyowataka. Mkataba ni makubaliano rasmi ya maandishi baina ya pande mbili. Kwa muktadha huu ni kati ya wachezaji wanaosajiliwa na vilabu vinavyowasajili.

Wanaosajiliwa wahakikishe wanalipwa fedha taslimu za usajili na kutokubali kulipwa kwa mafungu. Aidha vilabu lazima vifanye usajili makini na kufuata mkataba ili kuepuka malalamiko na kushitakiwa na wachezaji kwa kutolipwa mishahara kila mwezi.

Wachezaji ni waajiriwa yaani wafanyakazi kama wengine.

Vilabu vinaposhindwa kulipa mishahara ya wachezaji wao kila mwezi wataendeshaje maisha yao ya kila siku? Matokeo yake ni wachezaji kucheza wakiwa na dukuduku (joto la moyo linalosababishwa na kuudhika) kwa kutolipwa mishahara yao ya kila mwezi.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Kabudi ateta na mabalozi wateule

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, jana alikutana na kufanya mazungumzo na kupokea nakala za hati ya utambulisho za Balozi Mteule wa Algeria, Ahmed Djellal na mwenzake wa Ujerumani, Regine Hess.

Kabla ya kukabidhiwa nakala za hati za utambulisho kukoka kwa mabalozi hao jijini Dar es Salaam jana, Prof. Kabudi, alifanyaa mazungumzo na mabalozi wateule ambayo yalilenga kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na nchi zao.

Kabudi alimweleza Balozi Djellal Tanzania na Algeria zimeendelea kuwa na uhusiano mzuri na wa kihistoria tangu miaka ya 1960 wakati wa harakati za ukombozi wa Afrika dhidi ya ukoloni.

"Misingi ya uhusiano wa Tanzania na Algeria ilijengwa na waasisi wa mataifa haya mawili, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Ahmed Ben Bella wa Algeria," alisema Prof. Kabudi.

Waziri Kabudi aliongeza kuwa Algeria imeendelea kuwa na ubalozi wake Tanzania tangu mwaka 1964 ikiwa ni miongoni mwa nchi za mwanzo kabisa kufungua ubalozi nchini.

Mwaka 1981 nchi hizo zilianzisha Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) ambayo imechangia kuimarisha na kukuza ushirikiano katika masuala mbalimbali yakiwamo diplomasia, ulinzi, elimu, madini, nishati na michezo.

Kwa upande wake, Balozi Djellal aliahidi kuwa serikali ya Algeria itaendeleza ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Tanzania hususan diplomasia, kukuza na kuimarisha biashara, uwekezaji na utalii.

Katika mazungumzo na Balozi Hess, mteule huyo alimweleza Waziri Kabudi kuwa uhusiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na Ujerumani ni mzuri na kuongeza kuwa jukumu lake kubwa kwa sasa ni kuendeleza uhusiano huo.

Balozi Hess alisema kuwa mbali na uhusiano wa kidiplomasia uliopo kati ya Tanzania na Ujerumani, ushirikiano mzuri uliopo wa uwekezaji, biashara, utalii na elimu utaendelea kuimarika na kutoa zaidi fursa za maendeleo kwa Tanzania.

"Kuna baadhi ya wawekezaji kutoka Ujerumani ambao wameshaonesha nia ya kutaka kuwekeza Tanzania, hivyo nitawasiliana nao na kujua wamefikia wapi kwani Tanzania ina sifa nzuri.

Jukumu langu nikiwa Balozi hapa ni kukuza na kuendelea kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya Ujerumani na Tanzania, hivyo nitajitahidi niwezavyo kufanikisha jukumu hilo," alisema Balozi Hess.

# Mgogoro waibuka mchanga wa almasi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa almasi wanaounda vikundi vinavyotarajia kupokea marudio ya mchanga udhaniwao kuwa na madini kutoka Mgodi wa Williamson Diamond Ltd, wametofautiana na serikali kupitia Tume ya Madini kuhusu mgawanyo wa asilimia za tozo za madini hayo.

Kwa mujibu wa wachimbaji hao, tozo hizo zimelenga kunufaisha baadhi ya watu na si wachimbaji wadogo.

Wakizungumza kwenye kikao cha kuvitambua vikundi vitakavyopewa marudio hayo, kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Songwa, chini ya Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabanga Taraba, wachimbaji hao wamegomea baadhi ya tozo hizo. Baadhi ya wachimbaji hao, akiwamo Onesmo Jidawa, wamelalamika kutoshirikishwa katika mchakato mzima wa mgawanyo wa asilimia huku wakidai asilimia 70 iliyotengwa kwa ajili ya mkandarasi anayetengeneza barabara na eneo la kuhifadhia mchanga huo, chini ya Mbunge wa Kishapu, Seleman Nchambi, ni kubwa na itamnufaisha mwenyewe na si wachimbaji wadogo kama ilivyokusudiwa.

"Sisi hatutaki hiyo asilimia ni kubwa kwani wakati wanaipanga hawakutushirikisha. Tunaomba serikali ikae upya itushirikishe tupange kwa pamoja kila kundi linufaike kuliko hivi sasa linanufaisha kampuni moja ambayo inamilikiwa na mbunge," alisema Jidawa.

Naye Ofisa Madini Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akiainisha tozo hizo, alisema asilimia 70 ambayo inakwenda kwa mkandarasi huyo imetokana na kukosa mtu wa kujitolea kufanya kazi hiyo ya ujenzi wa barabara na baadaye alipwe kutokana na upatikanaji wa almasi,

Kumburu alisema kupitia sheria ya madini na makubaliano na Chama cha Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Shinyanga (Shirema), asilimia 15 itakwenda kwa mchimbaji mdogo, asilimia 0.3 halmashauri, asilimia saba ofisi ya madini, asilimia 15 ya mwenye shamba, na 70 kwa mkandarasi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Taraba, aliwataka wachimbaji hao kuheshimu sheria, taratibu, na miongozo ya serikali ambayo imewekwa ili kufikia lengo lao na kwamba ambaye hayuko tayari kutii sheria hizo, anaweza kufanya shughuli zingine za kumwingiza kipato kikiwamo kilimo.

Hivi karibuni, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipokuwa kwenye ziara mkoani Shinyanga, alifanya mkutano na wachimbaji wadogo wa almasi wilayani Kishapu na kuagiza mchanga wa marudio ulioko kwenye mgodi wa Mwadui wapewe wachimbaji hao kabla ya Desemba 22, mwaka huu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Joyland iliyopo Same mkoani Kilimanjaro, wakimsikiliza mwandishi wa habari wa kampuni ya The Guardian Ltd, Aisia Rweyemamu, walipotembelea chumba cha habari cha magazeti ya Nipashe na The Guardian kujifunza namna ya uzalishaji wa magazeti hayo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri aagiza wanasiasa wamulikwe uvamizi misitu

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameitaka Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Tabora kuchukua hatua dhidi ya wanasiasa na watu wanaochochea wafugaji kuvamia maeneo yaliyozuiwa na kuwashambulia askari wa wanyamapori.

Amesema uvamizi huo umekuwa ukisababisha kuuawa kwa askari, akitolea mfano mauaji dhidi ya askari wawili katika Misitu ya Isawima walipokuwa wanawaondoa wafugaji katika misiti hiyo hivi karibuni.

Kanyasu alitoa agizo hilo jana, mkoani Tabora, alipozungumza na wafanyakazi walio chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na uongozi wa Mkoa wa Tabora.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini mgogoro wa Misitu ya Hifadhi ya Isawima umekuwa ukichochewa na kiongozi wa wafugaji ambaye ni kiongozi wa kisiasa katika eneo hilo wilayani Kaliua, jambo linasababisha askari kuvamiwa na kuuawa.

Kanyasu alisema ni vyema hatua dhidi ya kiongozi huyo zikachukuliwa ili kuwafanya watumishi wa Wizara ya Maliasi na Utalii na wengine ambao wanashughulika kulinda maeneo yaliyohifadhiwa, kufanya kazi katika mazingira salama.

Alisema watu wanaoendesha uvamizi na mauaji dhidi ya watumishi wanaolinda maeneo yaliyozuiliwa, watafutwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kanyasu alisema vitendo hivyo visipochukuliwa hatua kali, uvamizi utaendelea kutekelezwa na wanaoendekeza mauaji dhidi ya askari kujiona wako sahihi kufanya hivyo na kuendelea kuharibu maliasili. "Anapouawa mtumishi analinda maeneo yaliyozuiliwa na hakuna mtu anapiga kelele, lakini wavamizi wanapoondolewa na vibanda vyao kuchomwa, wanajitokeza watu kuwatetea na kupiga kelele, inasikitisha sana," Kanyasu alilalamika.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, alisema tatizo hilo limeshaundiwa Kamati ya Uchunguzi na wanatarajia kutoa majibu ya kilichobainika na hatua za kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Katika hatua, Kanyasu aliwaonya watu ambao wameanza kuvamia maeneo yalizuiliwa na kuendesha shughuli zao kinyume cha tangazo la Rais John Magufuli la kuruhusu vijiji 900 vilivyoko kwenye hifadhi kubaki ndani ya hifadhi.

Alisema tangazo la Rais Magufuli halikusema watu waanze upya kuingia katika maeneo mapya kwa mtanzamo kuwa ipo siku nao wataruhusiwa kuendelea na shughuli zao.

Kanyasu alisema watakaokutwa katika maeneo ambayo yamezuiliwa, watachukuliwa hatua na watahesabika ni wavamizi.

# Mbunge CCM akiri uchaguzi mgumu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, amekiri uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ulikuwa mgumu kutokana na baadhi ya ahadi kutotekelezwa.

Masele aliyasema hayo jana katika Kijiji cha Galamba, Kata ya Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, alipozungumza na wajumbe wa kamati ya siasa ya kijiji hicho na kukagua miradi ya maendeleo.

Alisema uchaguzi huo ulikuwa mgumu kutokana na upinzani kuwa na nguvu iliyochochewa na kitendo cha CCM kutotekeleza baadhi ya ahadi zake kwa wananchi.

"Kampeni za uchaguzi uliopita wa mwaka 2014 na 2015 zilikuwa ngumu kweli kutokana na baadhi ya ahadi zilikuwa hazijatekelezwa, lakini uchaguzi wa mwaka huu kazi imekuwa nyepesi, tumeshinda kwa kishindo," alisema.

"Hata kwenye uchaguzi mkuu mwakani, kazi itakuwa nyepesi sana, tutashinda kwa kishindo kwa sababu ahadi nyingi tumezitekeleza kwa wananchi," alitamba.

Mbunge huyo pia aliwataka wanachama wa CCM kuendelea kushikamana ili kuendelea kukijenga chama na kuwatumikia wananchi.

Alisema ataendelea kutekeleza ahadi mbalimbali alizotoa kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji, umeme na uboreshaji wa huduma za afya.

Diwani wa Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, Agnes Machiya, alidai Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, imetekelezwa kwa asilimia 90 katika kata yake hiyo.



Kiongozi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, Seleman Bishagazi (wa pili kushoto), akichangia mada katika semina ilioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake wa ngazi ya chini, ili waweze kutumia nishati mbadala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watanzania watakiwa kusoma vitabu kujiongezea maarifa

**Na Maulid Mmbaga**

WATANZANIA watakiwa kujijengea utamaduni wa kusoma vitaba ili kujiongezea maarifa na elimu kuhusu mambo mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na mwandishi wa kitabu cha 'Talk to God' (Zungumza na Mungu), Masija Buchafwe, wakati akifanya uzinduzi. Buchafwe ana Shahada ya Uzamili ya Uhusiano kwa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (Saut), alitafasiri vitabu viwili katika lugha ya Kiswahili kutoka Kingereza vya 'Think Big' na 'God Sent A Man'.

Alisema kwenye vitabu kuna maarifa mengi ambayo endapo mtu atayasoma na kuyaelewa, yana msaada mkubwa katika kupambana na changamoto za kimaisha.

"Nikitolea mfano wa hapa nchini, tofauti na miaka ya 1950 hadi 1970, Tanzania ya leo haina watu wenye kiu ya kusoma vitabu," alisema Buchafwe.

Aidha, aliwasisitiza wazazi na viongozi wa taasisi za elimu kuwahimiza na kuwaelimisha vijana juu ya faida ya kusoma vitabu.

"Kitabu hiki mbali na kuangazia mambo ya kiimani, lakini pia kimeangazia mambo ya biashara, siasa, uchumi na upendo ambayo yamekuwa muhimu katika kuchochea maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla," alisema Buchafwe.

## Wakulima pamba walipwa mamilioni

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

KAMPUNI ya kuchambua mbegu za pamba ya Biosustain Tanzania ya mkoani Singida, imefanikiwa kukusanya kilo 1,487,453 za pamba zenye thamani ya Sh. bilioni 1.785 kutoka kwa wakulima wa zao hilo mkoani humo.

Meneja uzalishaji wa kampuni hiyo, Paul Deogratius, aliiambia Nipashe jana kuwa kampuni hiyo pia imefanikiwa kulipa Sh. bilioni 1.784 kwa wakulima wa zao hilo kupitia vyama vya msingi.

Alisema kampuni hiyo inatarajia pia kuvilipa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) Sh. milioni 50.334 kama ushuru wa zao hilo ili navyo viende kuwalipa wakulima waliobakia kulipwa kupitia vyama vyao.

Kwa mujibu wa Deogratius, wakulima nao kwa upande wao watapaswa kulipa madeni ya pembejeo za kilimo yanayofikia Sh. milioni 40.305 kupitia vyama vyao, walizokopa katika kipindi cha msimu wa kilimo wa 2018/2019 ili fedha hizo zirudi kwa kampuni hiyo na Bodi ya Pamba (TCB).

Meneja huyo alisema kampuni hiyo imeshasambaza zaidi ya tani 94.4 za mbegu za pamba na itaendelea kusambaza mbegu kwa wakulima kulingana na mahitaji yao.

"Kampuni ina mbegu za kutosha za kupanda kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 na mpaka sasa mbegu zilizosambazwa kwa wakulima ni aina mbili; UKM08 - C1- tani 68.4 na UKM 08 - DAS -1C tani 26," alifafanua.

## Polisi wataja chanzo kifo Mkurugenzi wa Zam Zam

INATOKA UK. 3

upekuzi katika ofisi yake na kugundua kuwa hakukuwa na uharibifu wowote katika ofisi yake, hakuna wizi wowote wa mali.

"Upekuzi ulifanyika na lilikutwa begi dogo la nguo chache za safari, simu yake ikiwa imezima, tiketi ya safari, pesa katika pochi Sh. 260,000 na vitambulisho vyake.

"Mwili wa marehemu ulipelekwa Hospitali ya Rufani ya Dodoma na kufanyiwa uchunguzi na daktari na kuthibitisha kuwa kifo chake kimetokana na moyo kufeli na kushindwa kufanya kazi.

"Hata hivyo, Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi kupitia simu zake kubaini kama kuna taarifa za ziada, na watu wasitumie taarifa ya kifo hiki kupotosha umma au kuunda taarifa zenye upotoshaji kama zinavyoenezwa mitandaoni," Muroto alionya.



Familia iliyojitambulisha kuwa ni ya Mfinanga kutoka Arusha wakipata mlo kwenye eneo lililotengwa maalum kwa ajili ya kupumzikia na kula chakula watalii baada ya safari za kutembelea vivutio, familia hiyo, ilisafiri kutoka Arusha hadi hifadhini siku ya pili baada ya sherehe za Krismasi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Wasiojulikana wavamia na kujeruhi watu

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WATU wasiojulikana wakiwa wameziba nyuso zao kwa vitambaa vyeusi huku wakiwa wamebeba silaha za jadi, wamevamia shamba la mfanyabiashara, Itandumi Makere, mkazi wa Arumeru na kuwajeruhi kwa mapanga baadhi ya mafundi waliokuwa wakijenga nyumba.

Licha ya kuwavamia mafundi hao na kuwajeruhi, pia wamefyeka mazao katika shamba lake lililoko eneo la Madira wilayani Arumeru mkoani hapa. Tukio hilo, linahusishwa na chuki za ukabila limetokea juzi majira ya saa nne asubuhi. Kwa mujibu wa mafundi hao, watu 10 walivamia eneo hilo na kuanza kuwashambulia kwa kutumia silaha hizo na kuharibu eneo la ujenzi.

Mmoja ya mafundi waliojeruhiwa vibaya kwa kukatwa panga kichwani, Joseph Nanyaro, alisema walivamiwa na watu hao wakiwatuhumu mafundi hao kujenga eneo lisiloruhusiwa.

"Tukiwa tunaendelea na ujenzi, ghafla tulishtukia gari aina ya Toyota Landcruiser VX likisimama mbele ya eneo la ujenzi na walikuwa zaidi ya watu 10, baadhi yao wakiwa wameziba nyuso kwa vitambaa, waliteremka kwenye gari na kuanza kutushambulia," alisema Joseph.

Alisema pamoja na kumjeruhi kwa panga, watu hao walikatakata mipira ya maji kufukia msingi wa nyumba iliyokuwa ikijengwa na walitoboa mifuko ya simenti 15 na kuimwaga chini.

Mmiliki wa eneo hilo, Itandumi Makere, akizungumza kwa masikitiko, alisema alipata taarifa kutoka kwa mafundi wake kuwa kuna watu wamevamia eneo hilo na kuanza kuwashambulia huku wakiwalazimisha kufukia msingi waliokuwa wamechimba kwa ajili ya ujenzi.

Alisema kimsingi eneo hilo ni mali yake na alikabidhiwa kihalali na ana nyaraka zote za umiliki, hivyo ameshangazwa na wavamizi hao wanaodai kuwa haparuhusiwi kujengwa.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema matukio hayo hayakubaliki wilayani hapa kwa kuwa chokochoko hizo zinatokana na chuki za ukabila na kwamba kwa nafasi aliyo nayo, hatakubali matukio kama hayo yaendelee kujitokeza.

Muro alisema Jeshi la Polisi wilayani humo linawashikilia baadhi ya watuhumia wa tukio hilo na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

# Kijiji chatoa somo matumizi bora fedha

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

WANANCHI wa Wilaya ya Babati wametakiwa kuiga mfano kwa wakazi wa kijiji cha Vilima Vitatu wilayani hapa, ambao wamewekeza Sh. milioni 105, zilizotokana na mapato ya hifadhi ya misitu ilioko ndani ya kijiji hicho, hivyo kusaidia kujenga zahanati ya kisasa.

Licha ya ujenzi wa zahanati hiyo, pia wanakijiji wa eneo hilo wameanza ujenzi wa shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita ili kuwarahisishia wanafunzi kutotembea umbali mrefu kwenda kutafuta elimu.

Kutokana na uwekezaji huo, wananchi katika vijiji vingine vya Wilaya ya Babari na Mkoa wa Manyara kwa ujumla, wametakiwa kuiga mfano huo kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea zahanati hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahati, Hamisi Malinga, alisema serikali ya kijiji hicho inahitaji pongezi kutokana na matumizi mazuri ya fedha za mapato ya hifadhi.

Malinga alisema kijiji hicho kilitoa wazo la ujenzi wa zahanati hiyo kwa serikali na waliona wazo hilo ni zuri na walilifanyia kazi kuunga mkono na hadi sasa ujenzi umekamilika na imeanza kutoa huduma. Aliwataka wananchi kujijengea tabia ya kutunza fedha wanazopata katika miradi mbalimbali ili kusaidia jitihada za serikali katika uwekezaji kwenye sekta za afya na elimu.

"Naomba niwapongeze kijiji hiki kwa jitihada mnazofanya kuhusu maendeleo. Ni vyema wengine wakaiga mfano kutoka kwenu," alisema Malinga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Vilima Vitatu, Aboubakary Msuya, alisema eneo hilo la hifadhi lina ukubwa wa hekta 12,800 na mapato ya hifadhi hiyo hupatikana kupitia watalii wanaokwenda kutalii na kulala katika hoteli za kitalii. Alisema awali walianza kupata mgawo wa Sh. milioni 20 na baadaye ziliongezeka hadi kufikia Sh. milioni 40 na kwa sasa mapato yameongezeka mpaka Sh. milioni 105.

Pia alisema baada ya kukusanya kiasi hicho cha fedha, walianza ujenzi wa zahanati hiyo ambao inahudumia wananchi takribani 4,000 walioko kijijini hapo. "Eneo la hifadhi tunalitunza vizuri linalindwa kwa kutumia askari ili watu wasivamie na kuharibu misitu iliyopo ndani ya hifadhi," alisema Msuya.

Alisema serikali ya kijiji imetoa kipaumbele katika ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho ili kutatua tatizo la wanakijiji kwenda nje ya kijiji hicho kutafuta huduma za afya. Pia alisema kijiji hicho, kimekuwa mstari wa mbele kuangalia mahitaji muhimu ya wakazi wa eneo hilo ili kupiga hatua kimaendeleo.

# DC akerwa kauli maisha magumu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amewataka wanawake, vijana na wenye ulemavu kuacha kulalamikia maisha magumu wakati wameshindwa kuchangamkia fursa ya Sh. milioni 230 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya mikopo.

Chaula aliyasema hayo juzi kwenye tafrija ya Sikukuu ya Krismasi ya watoto yatima, wanaoishi katika mazingira hatarishi, wenye ulemavu na wazee iliyoandaliwa na Charles Mnyalu, mdau wa maendeleo wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani humo.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona bado watu walalamikia hali ngumu au kudai vyuma vimekaza wakati kuna fursa ya mikopo imetolewa, lakini jamii imeshindwa kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema wanawake, vijana na wenye ulemavu wajiunge kwenye vikundi na kuvisajili kupitia ofisa maendeleo ya jamii ambaye atawasaidia kuwaandalia katiba za vikundi bila kulipia gharama zozote.

"Na fedha zenyewe wala hazina riba. Mkikopa Sh. milioni 10 mnarudisha Sh. milioni 10, hivyo changamkieni fursa hizo acheni kulalamika kuwa maisha magumu wakati ninyi wenyewe hamjatumia nafasi," alisema Chaula.

Alisema kwa mwaka huu wanawake walitengewa Sh. milioni 73 na wakakopa Sh. milioni 33 wakati vijana walitengewa Sh. milioni 72, lakini wakakopa Sh. milioni 17 na wenye ulemavu walitengewa Sh. milioni 36.

Alisema katika kata 18 zilizoko kwenye wilaya hiyo, kuna vikundi 1,212 vya wanawake, 23 vya vijana na vitatu pekee vya watu wenye ulemavu.

Mnyalu ambaye aliandaa tafrija hiyo kwenye sikukuu ya Krismasi alisema wamejumuika pamoja ili kuwapa furaha wahitaji.

Alisema kwenye tafrija hiyo wamefurahia pamoja na watoto yatima, wenye uhitaji maalum, wazee na walemavu wa Mji Mdogo wa Mirerani.

"Watu wasione sisi tuna fedha nyingi sana kwa kuandaa tafrija hii hapana tumeona tufurahie pamoja na wahitaji hawa kama tulivyofanya kwenye sikukuu ya Idd," alisema Mnyalu.

Alisema pia wamegawa vifaa vya masomo kwa watoto hao ikiwamo madaftari, kalamu na nguo ili nao waone bado kuna wazazi wanawajali na kuwathamini hapa duniani.

# Waomba kupunguza uharibifu wa ngozi

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAFANYABIASHARA wanaonunua na kuuza bidhaa za ngozi mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kutekeleza kwa vitendo mkakati wake wa kupunguza uharibifu wa ngozi viwandani kutoka asilimia 60 ya sasa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Silvester Silayo, alisema juzi kuwa katika mkoa wa Kilimanjaro, takwimu zinaonyesha kati ya asilimia 40 na 60 za uharibifu wa ngozi unatokea kwenye machinjio.

Alisema uharibifu huo unasababishwa na ngozi kuoza kutokana na kukatwa vibaya au kutobolewa.

Mfanyabiashara mwingine, Zainudin Hamza, mkazi wa Hai, alisema kwa hali ilivyo sasa, kuna haja kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutekekeza kwa vitendo mkakati wake wa kupunguza uharibifu huo ili kuliteka soko la ngozi la Afrika Mashariki.

Mkakati huo unaotekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi unakwenda sambamba na usajili wa wachunaji wa ngozi.

Kuanzia Agosti, mwaka huu, serikali ilianza kutoa leseni hizo, huku ikieleza kuanzia mwaka 2020 haitaruhusu mtu ambaye hana leseni kumshika mnyama, wala kumchuna kama hajafuata taratibu za kisheria.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura, wakati wa mahojiano yake na Nipashe, alisema ngozi ambazo zinaingia katika mfumo rasmi wa biashara, serikali inapata kodi katika vipande milioni 1.5 kati ya vipande milioni 10 vinavyozalishwa.

Tanzania inazalisha ngozi za ng'ombe milioni nne kwa mwaka, ng'ozi za mbuzi milioni 5.6 na ngozi za kondoo milioni moja.

Alipotakiwa kujibu ombi la wafanyabiashara hao, Bura alisema uharibifu huo licha ya wachunaji kukosa elimu sahihi, pia unachangiwa na magonjwa ambayo yanaharibu ngozi.

# Mbunge kicheko fursa ufugaji samaki

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MBUNGE wa Same Mashariki, Naghenjwa Kaboyoka, amesema ujio wa mradi mkubwa wa ujenzi wa mabwawa ya samaki katika jimbo hilo utafungua fursa za kiuchumi kwa zaidi ya wananchi 3,000.

Kaboyoka alikuwa akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na miradi hiyo ya ubia inayotekelezwa na wananchi wa vijiji vinavyolizinguka Bwawa la Kalemawe na Halmashauri ya Wilaya ya Same.

"Kwanza nipongeze juhudi ambazo zimefanyika hadi sasa za kulifufua bwawa hili na namna ambavyo jamii imehamasishwa na kukubali kuingia ubia.

"Ujio wa miradi hii ya ujenzi wa mabwawa ya kufuga samaki naamini kabisa kwamba itafungua fursa za kiuchumi sasa katika ukanda huu wa milimani. Kazi iliyobaki ni kuwajengea uwezo wananchi wetu," alisema.

Mwezi uliopita, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alitangaza Kampuni ya Kalemawe Dam Investment Ltd inayomilikiwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bonde la Mto Pangani na vijiji sita kuanza ujenzi huo.

Kwa mujibu Senyamule, vijiji vilivyoko katika mradi huo ni Kalemawe, Ndungu, Makokane, Mgandu, Msufini na Karamba.

Alisema kampuni hiyo iko tayari kuanza ujenzi wa mradi wa samaki kwa kuchimba mabwawa katika kijiji cha Kalemawe.

"Kampuni hii itakuwa ya mfano kwa kufanya vijiji vifaidike moja kwa moja kwa kushirikiana kama mmiliki wa kampuni," alisema.

"UNCDF (Shirika la Kimataifa la Uwekezaji wa Mitaji) wamefadhili awamu hii ya kwanza ya ujenzi ambao utaalamu toka Norway utatumika kwa kuwa ni nchi inayotegemea uchumi wa samaki kwa kiasi kikubwa," aliongeza.




Watalii walemavu wa kutosikia na kuongea, Carmezina Gianreco (35) na Thomas Maurer (33), ambao ni mke na mume wakiwa nje ya lango la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara wakijiandaa kwenda kutalii ikiwa ni mpango wao wa kufanya "fungate" ndani ya hifadhi hiyo. Watalii hao walikuwa wakisoma ramani ya eneo la hifadhi wakiongozwa na mwongoza utalii kutoka Kampuni ya Ereg Advertures ya Arusha, alisema ni mara ya kwanza kupata wageni wa namna hiyo, lakini wanaelewa na kufurahia. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Upandaji miti waileta 'Same Mpya'

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MPANGO wa serikali wa kuinusuru Wilaya ya Same kuondokana na ukame umeanza kubadili sura ya ukanda wa milimani wa wilaya hiyo, baada ya wananchi wa Suji kujitosa kupanda miti kila kaya kando kando ya barabara.

Wananchi hao wamefikia uamuzi huo baada ya kujengewa uwezo na Shirika la Floresta Tanzania kuhusu uhifadhi wa mazingira unavyoweza kubadilisha mandhari ya ukanda huo wa milima.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Same,Rosemary Senyamule, alisema kasi ya wananchi kupanda miti kando ya barabara ya lami iliyojengwa na serikali inatia moyo na kwamba maofisa mazingira wamepelekwa kutoa elimu zaidi.

Zaidi ya miti 46,000 ya aina mbalimbali imepandwa na wadau wa mazingira katika wilaya hiyo mwaka huu.

Alisema katika vijiji na kata mbalimbali za wilaya hiyo, Shirika la Floresta Tanzania limeendelea kupanda miti katika maeneo ya kimkakati.

"Hiyo miti tunadhani kwamba licha ya kupendezesha barabara na kukinga mmomonyoko, pia itasaidia kukinga ajali na kusaidia kupunguza mabadiliko yatokanayo na athari za kimazingira," alisema Senyamule.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza maofisa watendaji wa kata na vijiji kuweka mpango kazi wa kupanda miti ili kutekeleza mpango mkakati wa mazingira wa wilaya na lengo la kitaifa.

Aidha, alisisitiza kuwa kazi kubwa siyo ya kupanda miti, isipokuwa kazi kubwa ni kuitunza na kuikuza.








Baadhi ya wananchi wakisajili laini zao za simu kwa njia ya vidole kutekeleza agizo la serikali la kusajili laini hizo, huku zikiwa zimebakia siku chache ambapo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itazima laini hizo ambazo hazijasajiliwa kwa vitambulisho vya Taifa ifikapo Desemba 31, mwaka huu. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# RC alitaka Jiji la Dodoma kuondoa urasimu uwekezaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuondoa urasimu na vikwazo dhidi ya wawekezaji wanaohitaji maeneo kwa ajili ya uwekezaji, hususani ujenzi wa viwanda.

Dk. Binilith Mahenge alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Kiongozi huyo wa mkoa pia aliuagiza uongozi wa jiji hilo kumpatia taarifa ya namna na hatua zilizochukuliwa dhidi ya malalamiko ya baadhi ya wawekezaji waliofika kuomba maeneo kwa ajili ya uwekezaji katika jiji hilo.

Maagizo hayo aliyatoa mbele ya wajumbe wa kamati hiyo, wakiwamo Spika wa Bunge, Job Ndugai na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Kessy Maduka, waliolalamikia urasimu wa utoaji wa ardhi kwa wawekezaji. "Wenzetu wa jiji bado kuna tatizo la utoaji ardhi kwa maeneo ya uwekezaji kwa wawekezaji nadhani hawa waandae 'paper' (taarifa) na watuletee kwenye kikao kijacho ili tuone ni namna gani wameshughulikia suala hili," aliagiza.

Dk. Mahenge alisema kuna baadhi ya wawekezaji wakubwa kutoka ndani na nje ya nchi ambao wameonyesha nia ya kuwekeza katika Jiji la Dodoma, lakini wamekuwa wakikumbana na urasimu kutoka kwa watendaji.

"Wizara ya Elimu wamepata eneo la ekari 200, sehemu ambayo wanataka kujenga chuo cha ufundi, lakini wanaambiwa walipe, sasa unajiuliza kwanini jiji wafikiri kupata mapato zaidi kupitia ardhi badala ya uwekezaji wa faida ya baadaye?" Alihoji. Awali, akichangia ajenda katika kikao hicho, Spika Ndugai alilalamikia ugumu wa upatikanaji wa viwanja katika jiji hilo, akieleza kuwa unasababisha gharama kubwa za ununuzi wa viwanja.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Maduka, akichangia katika kikao hicho alilalamikia urasimu unaofanywa na watumishi wa idara ya ardhi jijini humo katika utoaji maeneo kwa wawekezaji, hali ambayo imekuwa ikiwavunja moyo wawekezaji.

"Mkuu wa Mkoa, kuna wawekezaji wengi sana wamekuja na ukiwapeleka pale jiji, hata kuonwa tu ni shida, sasa hii ni changamoto (tatizo) kubwa na inarudisha nyuma juhudi za uwekezaji," alilalamika. Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe na Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Bartazar Ngowi, walidai taarifa hizo hazijawahi kuripotiwa, lakini wakaahidi kuzifanyia kazi ili kuhakikisha kila anayehitaji eneo anapatiwa kwa mujibu wa taratibu.

# Ranchi Kongwa kuzalisha ndama 3,200

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MENEJA wa Ranchi ya Kongwa, Raymond Lutege, amesema wamejiwekea malengo ya kuzalisha ndama 3,258 katika kipindi cha uzalishaji mwaka huu kutokana na majike wazazi 4,072 walionao.

Lutege amesema hadi sasa ndani ya miezi mitano ya utekelezaji wa bajeti hiyo, wamezalisha ndama 268, sawa na asilimia tisa ya lengo na upimaji mimba umefanyika na kuonyesha idadi ya majike 3,113 yanatarajiwa kuzaa.

Akizungumza na Nipashe juzi, meneja huyo alisema uzalishaji kwa kipindi cha miezi mitano umepungua kutokana na msimu wa upandishaji ulioanza Machi mwaka jana hadi Agosti.

"Uzalishaji utaanza kuongezeka kwa kasi kubwa kuanzia Januari hadi Juni kutokana na msimu wa upandishaji," alisema.

Aliongeza kuwa ranchi hiyo inaendelea kukabiliana na matatizo ya magonjwa mbalimbali hasa kipindi cha miezi mitano ya uzalishaji, ambapo wamechanja ng'ombe na mbuzi chanjo ya mapafu kulingana na kalenda ya udhibiti wa magonjwa.

Alisema ranchi hiyo ilipanga kuzalisha kondoo 258 kwa mwaka huu wa fedha kutokana na majike wazazi 287, hadi kufikia mwezi Novemba, walikuwa wamezaliwa kondoo 118 ambao ni sawa na asilimia 45 ya makisio.

Alisema pia walipanga kuzalisha nguruwe 260, kwa majike wazazi 28 kwa mwaka na hadi sasa wamezalisha 66 na vifo ni 13.

"Katika uzalishaji wa mbuzi, tulipanga kuzalisha 572, kwa majike wazazi 635, ndani ya miezi mitano ya uzalishaji tumezalisha mbuzi 112, sawa na asilimia 35 ya uzalishaji, mbuzi 92 wamechinjwa na 19, wameuzwa," alisema.

# Wakulima walia na ubora mbegu alizeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Wakulima wa Alizeti (SUFA) kimesema moja ya matatizo yanayowakabili wakulima wa alizeti ni ukosefu wa mbegu bora kwa ajili ya zao hilo.

Meneja wa Sufa, Stephene Henry, aliyasema hayo alipozungumzia msimu wa zao hilo ambao unakaribia kuanza.

Alisema wakulima wa alizeti wamejipanga msimu huu kuhakikisha wanapata mbegu bora ambazo zitaleta manufaa kwa wakulima.

"Moja ya matatizo makubwa yanayotukabili ni pamoja ukosefu wa mbegu bora za kisasa, tunaomba serikali iliangalie kwa ukaribu ili tupate mbegu bora," alishauri.

Hivi karibuni, Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), lilisema limejipanga kuanzisha jukwaa la wadau wa alizeti nchini ili kuokoa Sh. bilioni 600 ambazo hutumika kuagiza mafuta kutoka nje kila mwaka.

Meneja wa Mradi wa Agriculture Transforming Market, Ole Sikala, alisema moja ya mipango yao ni kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima.


Alisema wako kwa ajili ya kuhakikisha kilimo cha alizeti kwa wakulima wa zao hilo kinafanyika kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na serikali.

"SNV tunasimamia katika maeneo mawili; kilimo na mikopo, kwa hiyo tunajitahidi kuwa karibu na wadau hao ili kuwainua," alitamba.

Meneja wa (SUFA), Henry, alisema alizeti iliyozalishwa nchini kwa mwaka 2016/2018 ni tani 352,908 na akabainisha kuwa wakizalisha kwa tija, kuna uwezekano wa kuzalisha mafuta ya kujitosheleza kwa mahitaji ya ndani na ziada ya soko la nje.

Alibainisha kuwa mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 700,000 wakati hali ya uzalishaji wa ndani ilikuwa tani 210,000 mwaka jana.

Alisema asilimia 50 ya mafuta hayo huzalishwa na wasindikaji wadogo na wakubwa.





Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mama Asha Suleiman Iddi, akiyafungua mashindano ya kuhifadhi Quran kwa kinamama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuungwa mkono na Jumuiya ya Maendeleo ya Wanawake wa Kiislamu Pemba, yaliyofanyika Fiysabilillah Tablih Markaz Kaskazini Unguja.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mke wa Rais ashangaa uovu waumini wa dini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Asha Suleiman Iddi, amesema licha ya kuenea kwa elimu ya dini nchini, bado kuna wimbi la vitendo viovu miongoni mwa waumini.

Amesema ni vyema dini iendelee kuota ndani ya vifua na mioyo ya waumini ili iwe kinga madhubuti ya kuyaepuka matamanio ya nafsi yanayoleta baa na fadhaa kwa jamii.

Aliyasema hayo wakati akifungua mashindano ya kuhifadhi Quran kwa kinamama wa Mkoa Kaskazini Unguja walioungwa mkono na Jumuiya ya Maendeleo ya Wanawake wa Kiislamu Pemba.

Alisema ipo mifano hai inayoonyesha waumini, hasa walezi kukimbia jukumu lao la ulezi, akitolea mfano wimbi la ongezeko la watoto wa mitaani.

Aliwakumbusha wazazi hasa kinamama kutenga muda wa malezi ya watoto wao licha ya mabadiliko ya harakati za kimaisha zinazotoa mwanya kwa 'wakorofi' kuwafanyia vitendo viovu watoto wao.

Alisema wimbi la udhalilishaji wa watoto wadogo mitaani kwa sasa limepamba moto na matokeo yake, mimba zisizotarajiwa zinashuhudiwa na kuleta sura mbaya machoni mwa waumini na jamii nzima kwa ujumla.

Aliwaahidi kinamama hao wa Jumuiya ya Kuhifadhi Quran Mkoa Kaskazini Unguja kuwapatia msaada wa kompyuta ili kuwa na uhakika wa kuhifadhi kumbukumbu zao za kila siku.

Akisoma risala, mmoja wa wanajumiya hao, Ukti Fatma Maruzuk, alisema yapo maendeleo makubwa yaliyopatikana tangu kuasisiwa kwa jumuiya yao miaka 11 iliyopita.

Fatma alisema mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la madrasa 100 zinazochipua wanachama wanaoongezeka kiwango cha ufahamu kutoka juzuu nne kwenda 19 na kwamba baadhi yao wamefikia juzuu zote 30.

Alisema jumuiya imefikia hatua ya kujitegemea kwa mahaji wake ambapo tayari hivi sasa imeshaanzisha mfumo wa ziara za kuzikagua madrasa zilizo na wanachama wa jumuiya hiyo ili kuangalia maendeleo yake.

Mlezi wa jumuiya hiyo, ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo, Vuai Mwinyi na Mlezi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kiislamu Wilaya ya Mkoani Pemba, Mmanga Mjengo Mjawiri, walisema ziara za mashindano ya kuhifadhi Quran kati ya Kaskazini Unguja na Kusini Pemba zinaleta faraja katika uhifadhi wa kitabu hicho kitukufu.

# ACT waipa neno Ofisi Usajili Matukio Jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii ichapishe vitambulisho vyote vilivyomo katika kanzi data yake ili wananchi waondokane na usumbufu.

Uongozi wa chama hicho umetoa ushauri huo baada ya kuwapo kwa malalamiko ya wananchi Kisiwani Pemba dhidi ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzazibari Mkaazi baada ya kuambiwa kuwa vitambulisho vyao havipo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mratibu wa ACT-Wazalendo Kisiwani Pemba, Said Ali Mbarouk, alisema Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii imeweka kituo kimoja cha kuchukulia kitambulisho, hali aliyodai imekuwa ikisababisha usumbufu kwa wananchi. Alisema baadhi ya wananchi wanaoishi mbali na kituo hicho hulazimika kuacha harakati zao za kiuchumi ili kufuatilia kitambulisho hicho.

"Kumtoa mwananchi masafa marefu kufuata vitambulisho ni tatizo kubwa na badala yake wawafuate wananchi katika shehia zao kama utaratibu wa awali uliotumika katika uandikishaji," alishauri.

Mratibu huyo pia aliitaka Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), kuendelea na ratiba yake ya uandikishaji wa wapigakura wapya na uhakiki wa wapigakura wa zamani hadi pale utolewaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi utakapokamilika kwa wananchi wote waliosajiliwa katika kanzi data Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii.

# Serikali yashtukia waganga wa jadi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Mkoa Kusini Unguja umeamuru kusitisha utoaji wa shughuli za tiba ya asili na kuondoka kwa kundi la waganga wa kienyeji katika Kisiwa cha Uzi hadi pake serikali itakapotoa maelekezo.

Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mahamoud, aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa kisiwa hicho baada ya kupokea malalamiko ya kushtumiana kwa imani za kishirikina zinazodaiwa kuchochewa na baadhi ya wazee kisiwani humo.

Alisema serikali imelazimika kuchukua hatua hiyo baada ya kubaini kundi hilo linajihusisha na utoaji wa tiba asili bila ya kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Alisema hali hiyo imesababisha kupandikiza chuki miongoni mwa wananchi na kuwapo kwa viashiria vya uvunjifu wa amani.

Alisema serikali haijakataza wananchi kujitibu kwa kutumia tiba ya asili katika kutafuta matibabu ya magonjwa yanayowasibu, lakini ni vyema kwa waganga hao kufuata sheria na taratibu zilizopo, tena bila ya kuathiri mila, silka na utamaduni wa nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Hamida Mussa Khamis, aliwataka wananchi kuacha jazba kwa kipindi hiki na badala yake kukaa pamoja na kuona wanalitafutia suluhu tatizo hilo kwa njia ya busara na amani.

Baadhi ya wazee wa kisiwa hicho walisema tangu kuingia kwa kundi hilo la waganga wa jadi, wamekuwa wakikumbana na madhila mbalimbali ikiwamo kudhalilishwa, kutishiwa maisha yao na hata kutengwa na jamii.



**CARD B, OFFSET WATIMIZA NDOTO YAO** Soma UK.19

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI DESEMBA 28, 2019



# 2020 HIYOOO

# Wasanii hawa kuingia mjengoni?

BASI SAWA

## Niki wa Pili wewe uligunduaje?

RAPA msomi na ambaye kauli zake zinaleta utata ndani ya jamii, Nikki wa Pili, wiki hii amezua gumzo baada ya kutoa mada ambayo inawagusa mabibi harusi.

Mwanamuziki huyo, aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba anashangaa kuona mabibi harusi wanajipodoa kwa vipodozi vingi siku ya harusi, lakini kimwonekano wanaonekana kutopendeza.

"Asilimia 80 ya mabibi harusi hawapendezi na makeup zao, lakini ni kama sheria lazima wapake," aliandika na kuibua mjadala katika mitandao ya kijamii.




## Wema, rubani waleta kigugumizi

MREMBO na malkia wa filamu nchini, Wema Sepetu, ameongeza kasi ya kuwachanganya watu mbalimbali baada ya kuposti picha ambazo zinaashiria yupo katika penzi zito na rubani.

Kwenye ukurasa wake wa Instagrama, Wema amekuwa na kawaida ya kurusha picha hizo bila ya kueleza chochote, lakini wambea wa mjini wanadai wawili hao ni wapenzi na wapo katika harakati ya kufunga ndoa.

Baadhi ya watu akiwamo Idris Sultan, wamejitokeza kutilia shaka penzi hilo na kutoa angalizo kwa rubani kwamba anatakiwa kuwa na moyo mgumu wakati wakipanga mambo yao.







# 2020 HIYOOO... Wasanii hawa kuingia mjengoni?

ZIMEBAKI siku mbili uingie mwaka mpya 2020, huku tukikumbuka raha na chungu ya mwaka unaomalizika 2019.

Wakati tunafikia ukingoni, ndani ya mwaka 2019 kuna mengi yamefanyika katika tasnia mbalimbali za sanaa, ikiwamo ukuaji wa muziki, mitindo na panda shuka ya wasanii mbalimbali.

Lakini kubwa zaidi ni pale baadhi ya wasanii kuamua kuingia katika siasa kwa kutangaza kuwania ubunge katika baadhi ya majimbo.

Wasanii walioweka wazi ni yao ni Harmonize ambaye ametia nia ya kugombea Jimbo la Tandaimba na Shilole yeye anakwenda kujaribu Jimbo la Igunga.

Hao ni wale wasanii walioamua kuweka bayana, lakini kuna wengi ambao wanatamani kugeukia katika siasa lakini kwa sasa imebaki kuwa siri yao.

Hivi karibuni wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa, Shilole, alisema ana nia ya kwenda kugombea ubunge kwa sababu anaamini anao uwezo wa kuwatumikia watu wake.

"Najiamini nina uwezo wa kuwatumikia watu wangu, mwaka 2020 nakwenda kugombea ubunge Jimbo la Igunga ili niwatumikie watu wangu," amesema Shilole.

Kwa upande wa Harmonize, yeye ameona kuingia katika siasa ili kukamilisha ombi la Rais Dk. John Magufuli, ambaye alipokuwa katika ziara ya mikoa ya kusini, alimwomba mwanamuziki huyo kugombea Jimbo la Tandahimba.

"Kama Rais Magufuli kaniomba nigombee ubunge mimi ni nani naweza kupinga, lazima nitafanya hivyo kwa sababu natii kauli ya kiongozi wangu," amesema Harmonize.

Hata hivyo, kuna tetesi kwamba kuna baadhi ya wasanii wakubwa watajitokeza kupigania nafasi hiyo ya kutunga sheria na kufanya mwaka 2020 kuwa wa kipekee.

Wasanii waliofanikiwa kuingia bungeni hadi sasa ni Joseph Mbilinyi, maarufu kama 'Sugu' Mbunge wa Mbeya Mjini na Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, anayefahamika kama Profesa Jay.

INSTA-TWITTER





**Habari** za kuniambia ukimaliza kazi huwa unapumzisha akili, wakati akili zenyewe hazipo hatupendi- **Dulla Makabila.**



**Humtumii** hata mese Hujihangaishi kumpigia simu, amekuelew Hata yeye akikutumia kujibu utafikiri unalazimishwa akikupigia unasema uko biz utamcheki baadaye, amekue lewa. Hivyo, utakapomuona yupo na mtu anayemtumia text mara kwa mara, anayer pigia simu kumjulia hali kuv na muda naye bila shaka na wewe utamwelewa- **Mwijaku**



## illan awa balozi hule za East Coast

ANAMUZIKi wa Bongo Fleva, Nillan, ameteuliwa a balozi wa shule za East Coast, katika kuhamasisha na kupenda elimu.

izungumza na BT, Nillan ambaye anatamba na o yake mpya 'Zombo' amesema nafasi hiyo imempa gamoto ya kuongeza uwezo katika kipaji chake ili ndee haki.

uwa balozi wa shule za East Coast inanifanya wakati nifikirie kukuza kipaji changu ili kuongeza awishi kwa vijana wapende kusoma. Naushukuru gozi wa shule kwa kuniona na kunikabidhi jukumu zito ambalo ni lazima nirudishe fadhila," amesema.





**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...

# Dogo Janja afikiria ndoa ya pili

RAPA maarufu nchini Dogo Janja, yuko mbioni kufunga ndoa na mpenzi wake mpya hivi karibuni.

Rapa huyo amesema kuwa kwa sasa amekuwa kimya kutokana na mambo ya kifamilia, lakini kuna jambo anatarajia kulifanya hivi karibuni. "Niko kimya kwa sababu ya majukumu, sasa nimekua, majukumu yameongezeka, mama mpenzi, kama hivyo." Amesema.

Rapa huyo kutoka Arusha aliwahi kufunga ndoa na mwigizaji Irene Uwoya, lakini haikuchukua muda ikavunjika.



# Madee akimbia mitandao ya kijamii

MADEE Ali, ambaye ni shabiki mkubwa wa Arsenal amesema kuwa akifungwa siku ya Jumapili dhidi ya Chelsea, hatoingia kwenye mtandao wake wa kijamii kwa siku tatu.

Amesema hatua hiyo inatokana na kuogopa 'domo' la Mwana FA ambaye ni shabiki lialia wa Manchester United.

"Kinachonikera kwa Mwana FA ni mdomo mdomo, nikifungwa tu nahama kwenye mitandao ya kijamii kwa siku tatu siingii." alisema Madee.



## INSTA-TWITTER

ji.
a.
,
e
e-
m-
wa
u.

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Anayeamini** ni bora kuliko asiyeamini hata kama anachoamini ni jiwe au mlima-**Jenifer Kyaka Odama.**



**Wewe** ndiyo ambaye umenisaliti. Nakwambia kuwa ulichofanya si sawa, unakuwa mkali. Ukanitelekeza nyumbani wiki nzima. Nimekudai talaka umenipa kwa njia ya simu. Kwa maana kuwa hata kuonana na mimi hukutaka. Naamua kuanza maisha yangu mapya, unanitafuta na wagambo na RB yako mkononi! - **Amber Rutty.**



**Ndio,** kuna tofauti ya elimu na akili, ila waliofanikiwa zaidi duniani ni wenye elimu na akili. Kati ya elimu na akili kwangu mimi bora akili. Nawajua wenye elimu wengi kazi yao mizinga tu 'town'. Na hapa simaanishi watu wasisome, la hasha! Tusome ila muhimu hiyo elimu iwe yenye akili, sio elimu ya vyeti isiyokufaa wewe na jamii yako - **Haji Manara**

Kuumbe!



## BRUCE LEE

# Jina lake lagombaniwa China

KAMPUNI inayosimamiwa na mtoto wa kike wa Bruce Lee, imeushtaki mgahawa mmoja maarufu nchini China kwa kutumia picha ya nyota huyo wa karate.

Kampuni hiyo kwa jina la Bruce Lee Enterprises, inadai kwamba mgahawa wa Real Kungfu, ilitumia picha hiyo katika nembo yake bila ruhusa. Kampuni hiyo inataka mgahawa huo kuondoa picha hiyo mara moja na inataka kulipwa fidia ya dola milioni 30 kama fidia.

Hata hivyo mgahawa huo, umejitetea kwamba serikali ya mitaa ya eneo hilo iliidhinisha matumizi ya nembo hiyo. Picha hiyo inamwonyesha mwanamume mwenye nywele nyeusi akiwa amesimama.

''Nembo ya mgahawa wa Real Kungfu, iliwasilisha ombi na kupatiwa baada ya ukaguzi wa kiwango cha juu uliofanywa na shirika la utoaji nembo, tumekuwa tukiitumia kwa takriban miaka 15 kufikia sasa'', kampuni hiyo ilisema katika taarifa yake iliyochapishwa katika mtandao wa kijamii wa Weibo.

''Tumeshangaa kwamba baada ya miaka mingi sasa tunashtakiwa, tunaisoma kesi hii kwa nguvu na kuandaa kutoa jibu letu.'' Iliongeza taarifa hiyo.

Mgahawa huo wa chakula uliopo katika mji wa Guangzhou, unaojulikana kama Zhen Gongfu kwa lugha ya Mandarin, ulianzishwa 1990 na sasa una zaidi ya matawi 600 nchini China.


Kampuni ya Bruce Lee Enterprises inasimamia biashara na haki za picha ya Bruce Lee.

Katika taarifa katika tovuti yake, kampuni hiyo ilisema imechukua jukumu la kuendeleza sanaa na filosofia ya Bruce Lee, ili kushinikiza ukuaji wake na maelewano duniani kwa lengo la kuendeleza mafanikio ya nyota huyo.


Kampuni ya Bruce Lee Enterprises, haikutoa tamko lolote ilipotakiwa kufanya hivyo.

Kesi hiyo huenda ikafuatiliwa kwa karibu baada ya serikali ya China kuahidi kulinda haki miliki.





IDRIS SULTAN



IRENE UWOYA

MENINA

# Hawa majanga tupu 2019

Na Adam Fungamwango

MWAKA 2019 unaelekea ukingoni, wapo ambao ulikuwa mzuri na wenye majanga kuanzia kwenye maendeleo hadi afya zao.

Hata hivyo, wapo wengi ambao haukuwa mwaka nzuri kwao kwa sababu mbalimbali kama magonjwa, balaa, mikosi, misiba, hata kimaendeleo na kuwasababishia ukosefu wa furaha na amani mioyoni mwao.

Hali hii si kwa watu wa kawaida tu, bali hata watu maarufu na wenye ushawishi kwenye jamii limewapata.

Leo tunawaletea mastaa ambao mwaka huu kwa namna moja au nyingine walipatwa na majanga ya aina mbalimbali na kuwasababishia matatizo.

**IDRISS SULTAN**

Aliitwa kwenye kituo kikuu cha polisi na kuhojiwa kwa mastaa kadhaa kabla ya kuachiwa kwa dhamana.

Hii ni baada ya kudaiwa kuweka picha yake na kuiambatisha na nembo ya Ikulu kwenye mtandao wake wa kijamii, kitu ambacho ni kosa kisheria.

Kutokana na tukio hilo 'lililotrendi' sana kwenye mitandao ya kijamii, lilimfanya Sultan ambaye ni mtangazaji, mwigizaji, mchekeshaji na mshindi wa shindano ya 'Big Brother' mwaka 2014, kuwa anakwenda kuripoti kituoni kila wiki.

**MWIJAKU MWEMBA BATONI**

Huyu ni msanii wa filamu na vichekesho pia, hivi karibuni aliingia kwenye janga, baada ya kudaiwa kusambaza picha chafu zinazodaiwa ni za mwanadada staa mwimbaji, Menina Atiki.

Baada ya picha hizo kuvuja na kila mmoja kuongea lake kwenye mitandao ya kijamii, Mwijaku alitakiwa kuripoti kwenye kituo cha Oysterbay na kufanyiwa mahojiano kwa saa kadhaa, kabla ya kuachiwa.

**IRENE UWOYA**

Staa huyu mkongwe wa filamu za bongo movie, na mmoja wa warembo wenye mvuto nchini aliingia au kujiingiza kwenye majanga mwenyewe mwaka huu alipowarushia noti waandishi wa habari na kusababisha uharibifu wa vifaa vyao vya kazi.

Hii ni baada ya baadhi ya waandishi kuacha shughuli iliyowapeleka hapo, ambapo wasanii waliwaita waandishi ili kuelezea wanachotaka kusema, lakini katikati ya mkutano, Irene Uwoya, bila kujua kuwa atasababisha matatizo, alirusha juu noti hizo zilizoanza kupeperuka na upepo na kuwafanya baadhi ya wanahabari kuanza kuziokota na kuachaka kazi iliyowapeleka, hivyo kuharibu utaratibu wote.

Pia ni kitendo ambacho kilitafsiriwa kuwa hakikuwa cha kiungwana.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), lilimwita na kumhoji, ikiwa ni pamoja na kumtaka kuwaomba radhi waandishi na akafanya hivyo.

**MENINA ATIKI**

Mwanadada mrembo, mwimbaji wa bongo fleva na mshereheshaji wa sherehe mbalimbali za harusi na kijamii.

Aliingia kwenye janga kubwa, baada ya picha chafu zinazodaiwa kuwa ni zake kuvuja na kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na kumsababishia matatizo makubwa kwenye jamii.

Kutokana na tukio hilo kuzidi 'kutrendi' mitandaoni, Baraza la Sanaa na Taifa (BASATA), lilimwita na kumhoji, kisha kuachiwa kuendelea na shughuli zake kama kawaida.

**AUNT EZEKIEL**

Mwanadada mrembo, mwigizaji mkongwe wa bongo fleva, naye aliingia kwenye majanga mwaka huu, baada ya kufungua 'pub' yake kali, lakini baadaye akaamriwa kuifunga baada ya baadhi ya watu wanaoishi karibu kudai inawapigia kelele. Hata hivyo Aunt Ezekiel mwanadada mpambanaji, hakukata tamaa na kuamua kutafuta haki yake, hadi 'pub' yake iliporuhusiwa tena kufanya kazi.

# IMETOKEA
# Babu aiba benki, awarushia watu pesa akiwatakia Krismasi njema

JE, ingekuwa wewe upo nje ya jengo la benki moja, kisha mzee mmoja anatoka ndani akiwa kashikilia bulungutu la fedha, tena akiwa hana wasiwasi ya kuporwa.

Ukiwa unawaza kwa nini mzee huyo anajiamini kutoka na fedha nyingi mkononi, ghafla anakugeukia na kukuliza "Unataka shilingi ngapi?

Kabla ya kumjibu, unashtuka kumwona mzee huyo anafanya tukio ambalo hata wewe linakushangaza, unamwona akichukua fedha zile na kuanza kuzirusha ovyo na zingine zikikurukia mwilini mwako.

Hapo nilitaka utafakari tu! Lakini kuna kisa cha kweli kimetokea huko Marekani baada ya bwana mmoja mwenye ndevu nyeupe alifanya uvamizi wa benki siku mbili kabla ya Krismasi na kisha kuzirusha juu.

Haikuwa kama bahati mbaya kwani mzee huyo alikuwa na furaha tele, huku akiwatakia kheri ya sikukuu ya Krismasi wapita njia.

Polisi wamethibitisha tukio hilo na kusema mwanaume huyo mzee wa kizungu alivamia benki ya Academy mjini Colorado Springs, Marekani siku ya Jumatatu.

"Aliiba pesa benki, akatoka nje na kuzitawanya kwa watu," shuhuda Dion Pascale alikiambia kituo cha Colorado's 11 News.

"Alianza kurusha fedha kutoka kwenye begi na kisha akaanza kusema, 'Merry Christmas!'"

Kwa mujibu wa mashuhuda, mtuhumiwa huyo aliwaacha watu wakipigana vikumbo kuwania noti hizo, huku yeye akapiga hatua chache kutoka benki na kuketi mbele ya mgahawa wa Starbucks, akisubiri kukamatwa.

Katika hali ambayo inaweza kuwa ya kustaajabisha kwa Wabongo, wapita njia wanaripotiwa kuwa walichota fedha zote zilizozagaa na kuzirudisha benki.

Ebu tujiulize tukio hilo lingetoa hapa Bongo, pesa hizo zingerudi tena benki? Jibu unalo wewe mwenyewe.

Hata hivyo, Polisi hawadhani kama babu huyo alipata usaidizi wowote hadi alifanikisha zoezi lake hilo.








## Hila Haijengi
## Mfitini anayejifisadi mwenyewe

**Na Adam Fungamwango**

FITINA na roho mbaya siku zote huwa havijengi. Watu wenye tabia hii mwisho wao huwa si mzuri.

Ndani ya jamii kuna baadhi ya watu wenye tabia ya kuwaonea kijicho wenzao wanaotafuta maendeleo ili wawakwamishe.

Filamu ya 'Hila Haijengi' imewaangazia watu wa aina hiyo na kutoa elimu kwa jamii kuachana na vitendo hivyo.

Imechezwa na wasanii nguli nchini kama Zuberi Huusein 'Niva', Mohamed Nurdin 'Chekibudi', Kephe Benny, Getrude Mwita, Seneta Abdallah na wengineo wengi.

Inaanza kuonyesha jinsi Niva akimpokea rafiki yake Chekibudi aliyetokea kijijini. Niva anafanya biashara ya kuuza bidhaa sokoni, ambayo ndiyo inayomfanya aishi mjini na kuendesha familia yake. Na ndiyo kazi ambayo aliyomwitia rafiki yake huko kijijini ili aje na yeye ajaribu bahati yake.

Kwa sababu bado ni mgeni, Niva ambaye anaishi nyumba ya kupanga, anampangia mwenzake chumba kimoja kwenye nyumba hiyo hiyo anayoishi.

Baada ya miezi mitatu tu, biashara ya matunda aliyoianzisha Chekibudi ikamwendea vizuri mno kuliko hata mwenyeji wake.

Kingine ni kwamba Chekibudi alikuwa mcheshi na mkarimu kitu ambacho kikasababisha kupendwa na wengi, lakini pia kuwa maarufu kwa muda mfupi.

Kitendo hicho kilianza kumuuma rafiki yake na kuanza kumwonea wivu.

Akaanza kumfitinisha kwa wateja na kila aina ya uovu, ili mradi tu mwenzake aonekane mbaya.

Baada ya kuona kwa kiasi fulani amefanikiwa, fitina ikahamia nyumbani.

Akawa anatangaza kwa wenzake kuwa Chekibudi ana uhusiano wa kimapenzi na mkewe na kwa sababu hiyo, akamshinikiza mwenye nyumba amtimue nyumbani hapo.

Kwa kuepusha ugomvi, Chekibudi alihama. Miezi mingi baadaye, hali ya Chekibudi ilibadilika. Maisha yake yalionekana kuwa mazuri tofauti ya awali. Alikuwa na gari, nyumba, akiendesha biashara kubwa tofauti na ile ya awali.

Habari zilimfikia Niva. Akaambiwa rafiki yake kwa sasa ni matawi ya juu.

Anaendesha biashara kubwa baada ya kupata mkopo Saccos.

Bila ushauri wake kufikiri na yeye Niva akaenda Saccos kukopa Sh. milioni 10, lakini badala ya kufanyia biashara, akapanga nyumba nzuri, akanunua gari na kufanya matanuzi makubwa yasiyo ya lazima.

Muda wa marejesho ulipofika hakurudisha hata senti tano, ikabidi wenyewe waliomkopesha kwenda kupiga mnada nyumba na gari kufidia pesa zao.

Mke wa Niva ambaye awali alipinga mpango huo, akaamua kuchukua chake na kuondoka kwao, akimuacha mumewe ambaye alikuwa hajui la kufanya.

Naye baada ya kuona hana lolote zaidi ya begi lenye nguo chache, aliamua kurudi kijijini na kumuacha rafiki yake aliyempokea Chekibudi akitamba.

Ingewezekana kama asingemfanyia fitina, angekwenda kumuuliza rafiki yake biashara gani anafanya hadi kufikia hapo alipo na yeye angemsaidia kuwa na maisha mazuri kama mwenzake.



MJENGO MPYA

# Card B, Offset watimiza ndoto yao



WANAMUZIKI maarufu ambao ni wanandoa, Cardi B na Offset, wamefurahia sikukuu ya Krismasi kwa kujinunulia jumba la kifahari kama zawadi.

Jumba hilo ambalo lina kila kitu ndani, eneo kubwa la bustani, maegesho ya magari na bwawa la kuogelea lipo katika Jiji la Atlanta, nchini Marekani. Cardi B amechukua ukurasa wake wa Instagram na kuweka video fupi inayoonyesha mandhari ya nyumba yao mpya.

Kulingana na maelezo ya rapa huyo, imewachukua miaka miwili kutafuta nyumba ambayo inaweza kuwatosha wao na familia yao.

Amesema nyumba hiyo inatosha kabisa kuishi na watoto wao wawili na nyumba nyingine za wageni zilizo jirani.

"Wakati umefungwa Offset na mimi tumepata nyumba nzuri ambayo tuliitafuta kwa miaka miwili kwa ajili ya kututosheleza na ya kifahari." Aliandika.

Ameongeza "Makazi yetu yatapunguza gharama, nyumba imependwa na Offset, tulikuwa na chumba ambacho akitoshelezi mahitaji yetu, sasa mume wangu ameafiki kuwa na makazi haya mapya."

Kutokana na posti hiyo, mashabiki wake waliwapatia pongezi wanandoa hao kwa kupiga hatua kubwa ya kumiliki nyumba ya kifahari.

Siku chache zilizopita Cardi B alifanya mambo ambayo yatakuwa katika kumbukumbu kwa kuwazawadia magari mume wake Offset na dada yake.

Cardi B alinunua gari aina ya G Wagon kama zawadi kwa dada yake ambaye alikuwa akitimiza miaka 24.



# Waongozaji bora 2019 Nigeria

MWAKA huu kila mwongozaji wa filamu amekuwa akisifiwa kulingana na aina ya kazi zake nzuri, wapo waliofanya vizuri kuanzia mwaka 2018.

Ramsey Nouah, ametajwa kuwa mwongozaji bora wa mwaka 2019, kutokana na filamu yake inayoitwa 'Living in Bondage au Breaking Free.'

Wengine waliofanya vizuri ni Niyi Akinmolayan 'The Set Up', Ishaya Bako '4th Republic', Akinyemi Sebastian Akinropo 'Coming from Insanity' na Kunle Afolayan 'Mokalik'.



## Solidstar anusurika kifo

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Solidstar amenusurika kifo baada ya kunywa kiwango kikubwa cha dawa za kulevya na kuzidiwa.

Nyota huyo alitumia akaunti yake ya Instagram siku ya Jumanne na kueleza jinsi alivyonusurika kifo kutokana na tukio hilo.

"Pale ni mstari wa kufa au kupona, ni bahati ilipotokea baada ya kunywa dawa kiwango cha juu siku chache zilizopita," alisema Solidstar.

## Kumechafuka wasanii hawa hawaivi

HALI ya hewa imechafuka! Ndivyo watumiaji wa mitandao ya kijamii wanaamini kuwa hivyo baada ya washiriki wawili wa Big Brother Nigeria, kuhamishia bifu lao uraiani.

Washiriki hao Nina na Tacha sasa wanaendelea kutimuliana vumbi kwenye Twitter na kusababisha mashabiki wao nao kuvurugana kisawasawa.

Aliyeanza kumchokoza mwenzie alikuwa Nina ambaye alitweeti kwa kulifananisha gari la Tacha ambalo alipewa kama zawadi ya siku yake ya kuzaliwa siyo jipya bali ni mtumba.

Bila kupepesa macho, Nina aliandika "Ninavyoliona hili Benzi ni mtumba, nashangaa limenunuliwa upya,"

Kauli hiyo iliwachefua mashabiki wa Tasha na kuanza kumporomoshea maneno makali na wengine kumuita kama mwanamke mwenye wivu.





## Wizkid atoa siri albam yake mpya

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, Wizkid, amesema baada ya kutambulisha albam yake 'Made In Lagos' sasa anakuja na nyingine ambayo itakuwa moto mkali.

Akitumia akaunti yake ya Twitter, nyota huyo amesema albam hiyo mpya itabeba jila la 'Wizkid' na kueleza ndani kutakuwa na nyimbo ambazo tayari amezitambulisha na zingine bado hajazitoa hadharani.

"Baada ya ' Made in Lagos! Nakupeni albamu yangu ya mwisho inayojulikana kama Wizkid ," aliandika.

## Mercy amaliza mwaka na '77 Bullets'

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Mercy Aigbe, anamaliza mwaka 2019 kwa kuipua jikoni filamu yake mpya inayoitwa '77 Bullets'.

Mercy Aigbe, ametambulisha filamu hiyo katika akaunti yake ya Instagram na kuwataka mashabiki wake wataiona siku chache kabla ya Mwaka Mpya.

Filamu hiyo yenye maudhui ya upiganaji, inahusisha genge la kihalifu ambalo linahangaisha jamii ya Yoruba.



SAFU



Na John Juma
0716217615

MIONZI YA SHERIA

# Faida ya kuunda kampuni ya umma, badala ya binafsi

KAMPUNI ya umma ndio huitwa 'Public Company' kwa lugha ya Kiingereza. Kampuni hutofautishwa na binafsi (Private Company). Zote ni kampuni kwa ajili ya biashara na mara zote hutegemea unahitaji kufanya nini, ili ujue ni kampuni ipi uunde.

Watu wengi wanadhani kuwa jina la kampuni hii 'umma' basi wanahisi inaundwa na serikali.

Neno umma ni jina na limetokana na namna muundo wake ulivyo, yumkini halina uhusiano wowote na kampuni za serikali.

Hivyo, yafahahamika kuwa, hata mtu binafsi mjasiriamali, wa kawaida anaweza kuunda kampuni ya namna hiyo, pengine kutokana na faida zinazotokana na kampuni ya aina hii.

**KWANINI UMMA?**

Uhuru wa wanahisa kwa wakati ni kampuni binafsi inaruhusu kuwa na wanahisa mwisho ni 50. Kampuni ya umma haina ukomo wa idadi ya wanahisa. Hiyo, maana yake waweza kuwa na wanahisa hata milioni na zaidi.

Hakuna ukomo wa kiwango cha mwisho, isipokuwa kuna ukomo wa kiwango cha chini. Kiwango cha chini yalazimu wanahisa kuanzia wawili.

Uhuru wa kuuza na kununua hisa, katika kampuni binafsi, hakuna uhuru wa kununua na kuuza hisa, kwa maana kabla hawajauza hisa, mtu apate ridhaa ya wanahisa wenzake. Wakikataa hawezi kuuza hisa hizo.Pia, wanahisa hawawezi kumuuzia hisa mtu ambaye wanahisa wengine hawampendi. Ruhusa ni kwa wanayempenda na kumridhia, ndipo anaweza kumuuzia na si vinginevyo. Hiyo ni tofauti na kampuni ya umma, ambako mmiliki wa hisa anachagua nani amuuzie hisa. Hakuna yeyote kati ya wanahisa wenzake anayeweza kumzuia kuuza hisa zake. Kwa haraka, unaweza kuona kuwa katika kampuni ya umma, uuzaji na ununuzi wahisa ni biashara huru inayotokana na uamuzi wa mtu.

Kuna suala la uhuru wa kutangaza hisa katika soko la hisa.

Katika kampuni binafsi, hakuna ruhusa ya kutangaza uuzaji hisa katika soko la hisa. Soko la hisa Tanzania ni moja tu; Soko la Hisa Dar es salaam ( DSE).

Wakati kampuni ya umma ruhusa iko wazi mtu anaweza kutangaza hisa zake na watu wanaoona kampuni yako inaweza kufanya kazi na ina mwelekeo mzuri, wanaweza kununua hisa na hivyo kampuni kukua na kujiimarisha.

**JINA**

Sheria inataka kila jina la kampuni ya umma kuishia na neno Public Limited Company (PLC). Itaanza na jina lolote ulilochagua, lakini mwisho lazima iishie hivyo. Mfano KR Public Limited Company au Kop Public Limited Company nk.

Utakuwa umewahi kuona huko mitaani neno PLC katika mabango ya kampuni mbalimbali. Hili humaanisha Public Limited Company na sio hiari kuweka bango hivyo, bali ni lazima.

Baadhi ya kampuni ya umma hapa Tanzania ni kama benki za CRDB na NMB nk, kwa kutaja chache.

Hata wewe waweza kuunda kampuni ya namna hii kwa faida nilizotaja na nyingine ambazo sikutaja.

# Ukifuata mbinu hizi, utapata maarifa


Na Mwandishi Wetu

KATIKA dunia ya sasa kila kitu kinahitaji maarifa ili kuvuka daraja moja la maisha hadi lingine.

Hakuna taifa au mtu mmoja mmoja ambaye anaweza kusema amepta mafanikio pasipo kuwekeza katika elimu.

Watu wote wanaofanya vizuri katika nyanja zote, huwa wana nidhamu kubwa ya kukusanya na kutumia maarifa. Maarifa kwa maana yake ni kwamba hali halisi za maisha na taarifa zilizotakana na elimu.

Mwanasayansi Albert Einstein aliwahi kusema "Katika zama hizi za habari, kuwa mjinga ni suala la uchaguzi". Hivyo, katikati ya taarifa hizi nyingi, chagua maarifa.




**KUSOMA**

Kusoma kunahusisha vitabu, magazeti na makala nyingine nyingi. Kusoma ni njia nzuri na ambayo inapendekezwa katika kuongeza maarifa.

Kupitia kusoma utashiriki katika maarifa na watu walio mbali na wengine hawako hai.

Watu wengi mashuhuri wameeleza namna wanavyosoma vitabu ili kuongeza ufahamu. Bill Gates anasoma kitabu kimoja kila wiki, Oprah Winfrey anasoma zaidi ya kitabu kimoja kila mwezi. Pamoja na watu wengine wengi kama Warren Buffett.

Kuwa na lengo la kusoma vitabu hasa kwa eneo unalotaka kujiimarisha. Soma vitabu pia kuhusu masuala mengine ya msingi. Kuwa mtu unayehabarishwa kwa kusoma habari muhimu za kitaifa, kibiashara na taarifa zote za muhimu.

Kama hujaanza kusoma, anza kwa kuweka lengo la kusoma vitu. Chagua kitabu cha kuanza nacho. Soma kurasa chache kwa kadri unavyoweza kuzimudu. Weka muda maalum wa kusoma. Jizoeshe kusoma ukiwa kwenye foleni au unasubiri kitu kingine, tumia vizuri muda ambao unakaa ukingoja kitu kingine.

Unaweza kujiunga na jamii ya watu wasomao. Unaweza kujiunga kuwa mwanachama wa maktaba.

Katika kusoma pia, fuatilia blogs na makala nyingine za waandishi wa mtandaoni. Chukua muda kusoma hizi makala ili kuongeza maarifa.

**SEMINA NA KOZI**

Pamoja na mbinu za kujifunza mwenyewe, semina na kozi zina umuhimu mpana hasa katika maeneo yanayohitaji utaalamu. Hudhuria semina zinazokupa fursa za kuongeza maarifa.

Chukua kozi fupi ama ndefu ili kuongeza maarifa katika eneo unalotaka.

**KUJIFUNZA KUTOKA KWA WATU WENGINE**

Ralph Waldo Emerson aliwahi kusema "Siri ya Mwanazuoni makini ni hii, kila mtu unayekutana naye ni mtaalamu katika eneo fulani, na kwa hilo inabidi ujifunze kutoka kwake."

Tunaishi na watu, walio na ufahamu, tuna nafasi pana ya kujifunza kutoka kwao. Uliza namna walivyofika hapo walipo, ulizia uzoefu wao pamoja na changamoto walizopitia.

Tafuta 'msimamizi' anayeweza kuwa mwalimu na mshauri katika nyanja mbalimbali za maisha. Hata kwa kufuatilia mienendo ya watu, tunaweza jifunza mambo mengi na kujiongezea maarifa.

**VIDEO, 'AUDIOBOOKS' NA KANDA**

Moja kati ya mwalimu mpya kabisa katika zama hizi za sayansi na teknolojia ni YouTube. Kupitia YouTube unaweza kujifunza juu ya kitu chochote unachotaka kujifunza na kuongeza maarifa, ufahamu na ujuzi katika maisha yako.

Kuna wakati ambapo huwezi nafasi ya kuchukua kitabu mkononi mwako, unaweza kutumia 'Audiobooks', hivi ni vitabu vilivyorekodiwa kwa njia ya sauti.

Pamoja na 'Audiobooks', zipo kanda nyingine nzuri zinazoelezea mada mbalimbali. Unaweza kuwa unasikiliza hizi wakati ukiwa unafanya kazi, ukiwa kwenye gari ama ukiwa unafanya mazoezi.

Kujifundisha mwenyewe

Barack Obama akiwa Mwalimu wa Sheria kabla hajawa seneta, aliwahi kusema "Kufundisha kunakufanya uwe mtu makini".

Dhamira ya kujiongezea ufahamu ili kuwafundisha wengine huongeza chachu ya kusaka zaidi maarifa na hivyo kuongeza ufahamu mpya juu ya ule uliokwisha kupatikana.

Unapofundisha wengine na ukiwa umenuia kuwa mwalimu bora, unatumia kila nafasi na fursa inayopatikana ili kuongeza ufahamu.

**JARIBU VITU VIPYA**

Pendelea kujaribu vitu vipya na ambavyo ulifikiri kwamba hutaweza. Katika kujaribu vitu vipya, tunapata uzoefu mpya ambao hujenga ufahamu mpya, na kutuongezea maarifa hivyo kuongeza kujitofautisha kwetu.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**

# KUKUMBATIANA

# Utamaduni unaodumishwa Rwanda

**Na Mwandishi Wetu**

KUKUMBATIANA ni ishara kuu ya kupeana maamukizi, kutakiana heri na urafiki kwa watu wa jamii mbalimbali barani Afrika.

Lakini kwa wananchi wa Rwanda, salamu ya aina hiyo imekuwa ya kipekee ikiwa ishara ya furaha na upendo miongoni mwa watu wa jamii hiyo.

Hata hivyo kuna baadhi ya jamii wanaona jambo hilo si la kawaida kwani huondoa heshima na madaraja kwenye jamii husika.

Wanyarwanda wanadumisha mila hiyo na kuona ufahari salamu ya kukumbatiana na kuifanya kama alama yao pale wanapotoka nje ya nchi hiyo.

**NANI ANAKUMBATIWA?**

Kukumbatiana katika utamaduni wa Wanyarwanda ni ishara ya upendo na furaha kutoka ndani ya moyo mtu anaionyesha kwa mwingine.

Salamu hii ambayo ni ya jadi imekuwa ikiendelezwa kizazi hadi kizazi, na huambatana na maneno kama vile "Amashyo" ambapo anayekusalimia hukutakia kuwa na ng'ombe wengi na "Yezu Akuzwe" akimaanisha "Yesu atukuzwe" na maneno mengine mengi ya kutakiana kheri.

"Utamaduni wa Wanyarwanda ni ishara ya upendo na furaha ya ndani ya moyo ambayo mtu anakuwa nayo kwa mtu mwingine", anasema mtaalamu wa masuala ya utamaduni nchini Rwanda, Profesa Malonga Pacifique.

Mtu anaweza kumkumbatia mpenzi wako, baba yako, ndugu yako awe wa kike au wa kiume, baba mkwe, mama mkwe, mme mwenza, rafiki au mtu mwingine yoyote yule pale unapomkuta katika tukio au mahali popote.

Mfano, kukumbatiana inaweza kufanyika katika familia, harusini, sokoni na hata njiani iwapo atakuwa na mtu unayemjua, hata kama binafsi haumfahamu.

Kiwango cha kumkumbatia kwa kawaida huwa ni sawa kwa kila unayemkumbatia.

**UTAMADUNI WA KALE NA SASA**

Kutokana na mabadiliko na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali za kigeni, baadhi ya Wanyarwanda wanaoishi maeneo ya mijini, wameanza kubadili mtindo wa salamu hii.

Baadhi wanajaribu kutosogeleana sana kimwili na wengine wakiiga salamu za kawaida za kisasa, kama kusalimiana kwa mikono au mabega hasa miongoni mwa vijana.

Hata hivyo wenzao wa maeneo ya vijijini bado wanaendelea na mila hiyo.

Profesa Malonga, anasema hata iweje salamu ya kukumbatiana kamwe haiwezi kupotea kwa sababu ya umuhimu wake katika utamaduni wa Wanyarwanda, huku akilinganisha na aina nyingine.

"Watu wengine wanakutana na kupeana mabusu, mwingine utamuona akiinama au anachuchumaa.

Kwangu mimi salamu hizo ambazo zinatajwa kuwa za kisasa naziona kama za 'kinafiki', anasema Profesa Malonga.

**VIJANA WANASEMAJE?**

Vijana hasa kutoka vyuo vikuu ambao walizungumza na BBC, wanasema kwamba kuna aina nyingi za salamu ambazo hukinzana na utamaduni, lakini si kwamba kukumbatiana hakupo tena.

Vijana wengi siku hizi wameiga salamu wanazoona kwenye filamu za Kimarekani, kusalimiana kwa mikono huku wakikutanisha mabega au pia kwa kugongeshana ngumi.

"Si kwamba tunapenda aina hizi za salamu, kufuata tu mambo ya kisasa kama tunavyoona kwenye filamu za Kimarekani." Anasema, Emmanuel Hakizimana (23) anayesoma Chuo Kikuu cha Elimu nchini Rwanda (KIE).

Emmanuel anakwenda mbali na kusema kwamba baadhi ya watu hivi karibuni wamekuwa wakiogopa salamu ya kukumbatiana au hata kupeana mikono kwa hofu ya kuambukizana magonjwa.

"Wakati mwingine watu wanaogopa magonjwa ya kuambukiza kama ebola hasa katika maeneo yaliyoko karibu na nchi ya Congo, utakuta kwamba kukumbatiana ni nadra sana siku hizi."



Salamu ya kukumbatiana ni ishara ya kuashiria upendo.



Vijana wakisalimiana kwa kugusana mabega. **PICHA ZOTE NA MTANDAO**

**WANASAIKOLOJIA WANAONAJE?**

Mtalamu wa Saikolojia, Grace Destiny, anasisitiza kuwa kukumbatiana ni zaidi ya salamu, kutokana na kwamba kukumbatia mtu kunafanya mawasiliano yanayowasilisha moja kwa moja hisia za upendo baina ya watu wawili. Destiny ambaye ni mtaalamu wa saikolojia ya uhusiano na familia, anasema kukumbatiwa ni ishara ya kukubalika na salamu hii zaidi ina manufaa kwa jinsia ya kike.

Mwanamke pamoja na mtoto wa kike wanahitaji kukumbatiwa na jinsia ya kiume na pale wanapokosa kukumbatiwa huwa wanakuwa na hisia tupu.

"Mtu anapokumbatiwa hujihisi kuwa na hakikisho la juu la usalama wake na hii hufanya atulie kiakili." Anasema mwanasaikolojia huyo kuwa wazazi wa kike na kiume wanapaswa kuwakumbatia watoto wao wanapokuwa, ili kuwaepusha na hisia za utupu ambazo watataka zijazwe na watu wengi. Akisisitiza juu ya umuhimu wa mgusano wa mwili kwa njia ya kukumbatiwa.

" Kukumbatiwa ni muhimu sana kwa mfano mwanamke ambaye ananyanyaswa na mume wake, anaweza kuliwazwa au kubembelezwa tu kwa kukumbatiwa na hiyo ikamfanya asahau unyanyasaji aliotendewa na mumewe," anasema.

Anaongeza msisitizo huo kwamba wazazi wa kiume wawakumbatie watoto wao wa kike kwani huwajengea uwezo wa kujiamini na kuhisi upendo wa wazazi wao wa kiume.

"Kwa jamii kama ya Wanyarwanda, kukumbatiana kunaimarisha hisia za umoja wa kijamii, na familia ya kibinadamu kwa ujumla, mgusano wa kimwili hasa kwa jinsia tofauti ni muhimu sana." Anasema, kukumbatiana hujenga hisia za udugu wa kaka na dada miongoni mwa jamii kama ya Wanyarwanda na kujihisi wako salama.

**MADHARA YAKE**

Hata hivyo, kukumbatia kunaweza kuleta madhara pale unapomkumbatia au kukumbatiwa na mtu mwenye maradhi ya kuambukiza kama vile ebola na mengine yanayoweza kuambukizwa kwa njia ya kukumbatiana au kusalimiana kwa mikono.

Kutokana na maambukizi ya ebola katika nchi jirani ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Wanyarwanda husussan wale wanaoishi katika maeneo yao wamekuwa na hofu ya kusalimiana au hata kukumbatiana na watu wasiowajua, licha ya kwamba salamu yao ya kukumbatiana ni vigumu kuiacha.

Na Mwandishi Wetu



Teresa Xu, raia wa China akiongea na waandishi wa habari kuhusu kuishtaki hospitali iliyomkatalia kugandisha mayai yake ya uzazi.

# Mwanamke aishtaki hospitali kukataa kugandisha mayai yake ya uzazi

TEKNOLOJIA inapozidi kupanuka, ndivyo watu wanakuwa na uhuru wa kupanga na kuamua mambo mbalimbali kwa uhakika ikiwamo suala la uzazi.

Kwa kutumia teknolojia ya kisasa, watu wanaweza kuamua lini wanataka kupata mtoto, wapi na jinsi gani ya mtoto wangependa kuwa naye.

Lakini kutokana na uwezo huo wa vifaa vya kisasa, mwanaume au mwanamke anaweza kuhifadhi mayai yake ya uzazi na kuamua kuyatumia wakati anaona unafaa.

Hata hivyo, matumizi hayo ya teknolojia yanaweza kuleta usumbufu katika jamii, kwani katika tukio la hivi karibuni mwanamke mmoja raia wa China ameishtaki hospitali moja baada ya madaktari kukataa kugandisha mayai yake ya uzazi.

Mwanamke huyo anadai hakutendewa haki hasa kutokana na majibu aliyopewa kwamba hajaolewa, jambo linalokwenda kinyume na sheria ya njia za uzazi zisizo asili.

Teresa Xu, aliwasili katika hospitali moja inayoshughulikia masuala ya kinamama mwaka uliopita, akiwa na nia ya kugandisha mayai yake katika kipindi ambacho anataka kuweka kipaumbele kwa taaluma yake.

Mwanamke huyo ambaye ni mwandishi huria mwenye umri wa miaka 31, anasema kwamba mhudumu wa hospitali hiyo, alimsihi apate mtoto badala ya kugandisha mayai yake. Baadaye akafahamishwa kuwa hawezi kuendelea na matibabu hayo.

"Nilikuja hapa kwa ajili ya kupata huduma ya kitaalamu, lakini badala yake nimepata mhudumu anayenisihi niachane na kazi yangu kwa sasa na kupata mtoto kwanza," Xu ameliambia shirika la habari la Reuters.

Chao Wei, msemaji wa hospitali, anasema kwamba hospitali hiyo ilikuwa inafuata sheria za serikali, chini ya teknolojia za uzazi wa njia zisizo za asili, kwa mujibu wa gazeti la New York Times.

Jumatatu, mahakama moja huko Beijing ilisikiliza kesi iliyowasilishwa na Xu, dhidi ya hospitali hiyo. Kesi hiyo ambayo inatarajiwa kuendelea kwa miezi kadhaa, imezua gumzo katika mitandao ya kijamii ya Uchina ambapo wengi wanamuunga mkono Xu.

Akizungumza baada ya kusikilizwa kwa kesi, Xu amesema "kwangu mimi sikuhisi kama niko mahakamani peke yangu. Kilichonijia ni kwamba nimesimama kupigania haki ya wanawake wengine wengi ambao hawajaolewa."

Yai la mwanamke linapungua nguvu yake kadiri anavyoendelea kuzeeka, na kufanya iwe vigumu zaidi kwa wanawake wenye umri mkubwa kupata mtoto. Kwa sasa hivi, ugandishaji wa mayai ni jambo ambalo linafanyika kwa wingi nchini China, huku wanawake wenye uwezo wakisafiri nje ya kupata matibabu hayo.

Mwaka 2013, mwigizaji wa kike maarufu wa nchi hiyo, Xu Jinglei, alitangaza kwamba amegandisha mayai tisa ya uzazi wake.

Jinglei, alisafiri Marekani akiwa na umri wa miaka 39 kupata matibabu ya uzazi wa njia zisizo za asili.

Xu, anasema alikuwa akitaka kwenda nje ya nchi kupata matibabu hayo, lakini imekuwa ghali mno kwake baada ya kuarifiwa kuwa gharama ya matibabu anayohitaji ni yuan 100,000 au yuan 22,032 nchini Marekani.

Watumiaji wengi wa mtandao wa kijamii wa Weibo walimuunga mkono mwanamke huyo kwa kutumia hash tag yenye maneno sawa na "Kesi ya kwanza ya kugandisha mayai ya uzazi kwa mwanamke ambaye hajaolewa".

Mtu mmoja ameandika "Uzazi hakustahii kuwa jambo pekee lenye kutathmni thamani ya mwanamke. Kando na kuwa mama, wewe ni mtu unayejitegemea."

"Ikiwa sheria za Uchina zitabadilika, na iwe huru kwa wanawake ambao hawajaolewa kuwa na hifadhi ya kugandisha mayai ya uzazi! Tatizo la idadi kubwa ya watu linaweza kutatuliwa baadaye. Bado kuna wengi ambao hawataki kuolewa, lakini wanataka watoto." Anaongeza mchangiaji mwingine.

Kumekuwa na sheria kali dhidi ya wanawake nchini China tangu kuanzishwa kwa sera ya upangaji uzazi miaka ya 1970. Ilibadilisha sera yake ya kuwa na mtoto mmoja hadi kuwa na watoto wawili mwaka 2015, lakini bado kuna sheria nyingi za matibabu ya uzazi.

Moja ya sera haiwaruhusu wanawake ambao hawajaolewa kugandisha mayai yao ya uzazi.

Baadhi ya watumiaji wa mtandao wa Weibo hatua hiyo na kuhoji kwanini mwanamke huyo anaishtaki hospitali. "Sidhani kama hospitali ina tatizo lolote katika uendeshaji wa shuguli zake. Anastahili kulishtaki Shirika la Taifa la Uzazi wa Mpango badala ya hospitali," mtu mmoja amesema.

**BBC.**



Kifaa maalum cha kugandishia mayai ya uzazi. **PICHA ZOTE MTANDAO**


## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 26 00)



Dondoo: Kulia
1. Dakitari
7. Silaha ya kufyatulia risasi
8. Mtu asiye raia
10.Anayejua zaidi
12.safisha mwili
14.Heshima
15.Nyanyasa
16.Patia majeraha
19.tembea kwa kufuatana
23.Mzoga 25.Gulio
26.Askari wa kirumi
29.Mpango wa kufanya mambo
20.Wingi wa neno mgodi
31.Mfuasi wa chama cha siasa
32.Mfalme wa Nyika
33.Mzazi

Dondoo: Chini
1. Bei ya kitu
2.Baraza kuu la waislamu nchini
3. Ushirikiano wa kibiashara
4. Kanya 5. Sala
6. kisu katika mtutu wa bunduki
9. mzunguko kamili mmoja
11.Shutumu 12.Shuhudia
13.Humaanisha Bibi Carrebean
15.Haribika na kutoa harufu
17.Mamlaka 18.Nyanyuka
20.Alifukuzwa kwa kujaribu kumpindua Mugabe 21.Msafiri
22.Msituni
24.Hufukiziwa
27.Sema Naam
28.Sujudia

Jibu toleo lililopita



# VITUKO KRISMASI & MTI KRISMASI

## ■Nyoka ajiviringisha katika mti
## ■Uwanja ndege waunda kwa visu
## ■Nigeria waliunda kwa chupa
## ■Waabudu ndani mahema porini



Mti wa Krismasi uliyovingirishwa na nyoka.

**Na Mwandishi Wetu**

NI kawaida, unapotaja Krismasi, huenda mtu anafikiria kutengeneza mti wake na mbwembwe zake nyingine sebule yako za upambaji.

Bila shaka hatarajii uwe mti unaoning'ing'ia visu, risasi na viberiti vya kuwashia sigara.

Uwanja wa ndege wa Vilnius nchini Lithuania, umefichua mti mbadala wa msimu wa sherehe za Krismasi, uliotengenezwa na vifaa vilivyokamatwa kutoka kwa wasafiri pekee.

Ni mti wenye urefu kima cha mitamoja na nusu na ilichukua wiki mbili kufanikisha namna ya kutengeneza hadi ukakamilika.

"Lengo ni kutuma ujumbe wa kuelimisha juu ya umuhimu wa usalama wa safari za anga," anasema Msemaji wa uwanja wa Ndege wa Vilnius.

"Vifaa hivi vinazuiwa kubebwa katika mabegi ya wasafiri ya mkononi na vilichukuliwa kutoka kwa wasafiri walipokuwa wakikaguliwa, visu, mikasi, viberiti vya kuwasha sigara na kila aina ya vifaa vingine hatari.

"Kwa hiyo, kama hautaki vifaa vyako vya kibinafsi, ambavyo vimezuiwa visiishie katika mti wa Krismasi ya mwaka ujao, ni bora uangalie masharti ya kubeba begi la mkononi unaloingia nalo kwenye ndege kabla ya safari yako," anasema.

Hiyo haishii katika Uwanja wa Ndege wa Lithuanian pekee, katika ubunifu wa mti wa Krismasi mwaka huu.

Kijiji cha Ullapool, kilichopo kwenye mwambao wa West Highlands, kimesimamisha mti wa mita tisa uliotengenezwa kwa nyavu za kunasia samaki.

Ni ubunifu unaotengeneza kwa vifaa hivyo vilivyoundwa kwa nyavu 340 zinazotumiwa kunasa samaki baharini-na ni mtindo wa hivi karibuni wa utamaduni wa Ullapoo, huko Scotland na ulioanza mwaka 2016.

Umaarufu wa kutotumia miti asilia inayotumiwa kwa ajili ya Krismasi, unaweza pia kupungua kwa watu ambao ni makini katika kuhakikisha sherehe za Krismasi zinaendana na haja ya kutunzaji mazingira yanayowahusu.

Kwa mujibu wa Shirika la Marafiki wa Dunia, zaidi ya miti milioni nane ya Krismasi hununuliwa nchini Uingereza pekee kila mwezi wa Desemba, ikiwa ni kiwango kikubwa kinachoweza kuathiri mazingira ya dunia, kadri uadhimishaji unavyopamba moto.

Njia mbadala ya kudumu ya kuhifadhi mazingira, inatajwa na wadau ni pamoja na kupanda miti binafsi ambayo mtu anaitunza na kisha anakodisha mti mmoja.

Katika Jimbo la Florida lenye jua kali nchini Marekani, ambako wastani wake kwa mwezi Desemba ni takribani nyuzi joto 22, timu ya mpira wa magongo iliamua kuvaa nguo za msimu wa baridi uwanjani wakati wa jua, yote ni sehemu ya mbwembwe za kusherehekea Krismasi.



Mti wa Krismasi ulioundwa na chupa.

**NYOKA AJIPINDA**

Ikiwa ni mwendelezo ya yatokanayo na Krismasi, nchini Australia, kuna mwanamke amegundua nyoka mwenye urefu wa mita moja (sawa na hatua moja ya mtu mzima mwenye urefu wa kati) aliyejipinda katika mti wa Krismasi.

Mwanamke huyo alipongundua hilo alihofu na kuomba msaada kumwondoa, katika nyumba yake huko Melbourne, Victoria Jumapili iliyopita.

Mtaalamu wa kushika nyoka, Barry Goldsmith, anasema kuwa nyoka huyo aliingia kupitia eneo la wazi katika mlango wa nyumba yake, kabla ya kujipinda katika mapambo ya mti huo kuunda makazi.

Nyoka huyo aina ya Tiger wanapatikana zaidi katika pwani ya Australia na wana sumu kali na Goldsmith anamsifu mwanamke huyo kuchukua hatua madhubuti baada ya kugundua uwepo wa nyoka huyo.

Ni simulizi zinazoendelea, huku kukikumbukwa rekodi ya mwaka 2015, Nigeria kushika nafasi ya dunia kwa kutengenezwa mti mkubwa zaidi wa Krismasi ikishika rekodi ya dunia, chupa za bia 1,000 zilitumika kuunda umbo hilo katika Kisiwa cha Victoria, jijini Lagos na kupiku kasi kama hiyo ya Wachina, nchini kwao.

**WALIOVUNJIWA KANISA**

Katka Jimbo la Aceh, nchini Indonesia Wakristo waadhimisha Krismasi kwenye mahema katikati ya msitu, kutokana na makanisa yao kuvunjwa mwaka 2015 na nyendo za wapinzani wao wa kiimani wenye msimamo mkali.

Makanisa yao yalishambuliwa na kuvunjwa na mamlaka hizo zinazodai Wakristo hao hawana kibali cha kujenga upya nyumba zao za ibada katika eneo hilo, jambo linalowakwaza kuibua tena makanisa kwa miaka minne sasa.

Indonesia ina katiba inayoruhusu uwepo wa dini mbalimbali, lakini katika uhalisia kuna misuguano.



Mti wa Krismasi ulioundwa na vifaa hatari vilivyokamatwa katika uwanja wa ndege. **PICHA: MTANDAO.**

## Uturuki kutuma vikosi Libya

**ANKARA,** Uturuki

UTURUKI itatuma wanajeshi nchini Libya kwa ombi la serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa mjini Tripoli.

Rais Recep Tayyip Erdogan amesema juzi kuwa kikosi hicho cha wanajeshi kitatumwa mapema mwezi ujao, hatua ambayo inaleta uwezekano wa kuimarisha mapambano ya kimataifa katika nchi hiyo ya Afrika kaskazini iliyoharibiwa kwa vita.

Serikali inayotambuliwa kimataifa ya Libya, imekuwa ikihangaika kuzuwia mashambulizi ya miezi kadhaa yanayofanywa na jeshi lililoko Mashariki mwa Libya linaloongozwa na Jenerali Khalifa Haftar.

Mwezi uliopita, Uturuki na kiongozi wa serikali ya Libya mjini Tripoli, Fayez al-Serraj, walitia saini makubaliano ya ushirikiano na makubaliano mengine kuhusu mipaka ya bahari katika eneo la Mashariki ya Bahari ya Mediterania, ambako Uturuki inakabiliana na mzozo.

Mzozo huo unahusisha mahasimu wake wa kikanda Ugiriki, Cyprus, Misri na Israel kuhusiana na kupata nafasi ya kumiliki maeneo ya maji yenye utajiri mkubwa wa gesi. **DW**

## Muungano wa serikali Ujerumani waingia ufa tena

**BERLIN,** Ujerumani

SERIKALI ya Ujerumani imetumbukia katika mzozo mpya na kutishia kuvunjika baada ya kuibuka tena na mzozo wa kuweka ukomo wa mwendo kasi wa magari katika barabara zake kuu.

Mzozo huo wa muda mrefu umezushwa tena kutokana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Wajumbe wa ngazi ya juu wa chama cha Social Democratic SPD, chama kinachoshiriki kuunda serikali inayoongozwa na Kansela Angeka Merkel, kimemshutumu Waziri wa Usafiri kutoka Chama cha kihafidhina cha CDU, Andreas Scheuer, kwa kuwa na tabia ya kuzuwia suala hilo.

Bunge la nchi hiyo limekuwa likikataa ukomo wa kuendesha magari kwa kasi, na Wizara ya Usafiri imesema inataka kudhibiti usafiri, kwa njia bora ya kidigitali na yenye nafasi kadhaa bila ya kupiga marufuku.

Lakini kiongozi mwenza aliyechaguliwa hivi karibuni wa Chama cha Social Democratic, Saskia Esken, amesema ukomo wa magari kwenda mbio katika barabara kuu ni muhimu kwa ajili ya kulinda mazingira na kusaidia usalama wa taifa. **DW**

# Ndege yaanguka yaua watu 14, yajeruhi 35

**NURSULTAN,** Kazakhstan

WATU 14 wamefariki baada ya ndege iliyokuwa na abiria 98 kuanguka nchini Kazakhstan.

Kulingana na maofisa wa uwanja wa ndege wa nchi hiyo, wanasema ndege hiyo inayomilikiwa na Kampuni ya Bek Air, ilianguka muda mfupi baada ya kupaa katika Uwanja wa Ndege wa Almaty, mapema jana.

Takribani watu 35, ikiwamo watoto wanane walipelekwa hospitali baada ya kujeruhiwa. Ndege hiyo ni ya aina ya Flight Z92100.

Mwandishi wa Reuters, alisema wakati ndege inapaa kulikuwa na hali mbaya ya hewa, huku kukiwa na ukungu mzito katika eneo la mkasa ijapokuwa bado haijulikani chanzo cha ajali hiyo.

**Ndege hiyo ilikuwa ikielekea katika mji mkuu wa Kazakhstan wa Nursultan, kutoka mji mkubwa wa Almaty.**

Ndege hiyo ilikuwa ikielekea katika mji mkuu wa Kazakhstan wa Nursultan, kutoka mji mkubwa wa Almaty.

Alisema ndege hiyo ilipoteza mawasiliano mwendo wa saa moja na dakika 22, kabla ya kugonga kizuizi kimoja na kuangukia nyumba ya ghorofa mbili.

Picha za waokoaji wakijaribu kuwasaka manusura katika eneo la mkasa huo zilisambaa, ndani yake kunasikika mwanamke akiita gari la wagonjwa.

Ndege hiyo haikuwaka moto baada ya kuanguka. Tume maalumu itaundwa kubaini chanzo cha kuanguka kwa ndege hiyo.

Rais wa Kazakhstant Qasym-Jomart Toqayev, alitoa taarifa ya kusikitishwa na mkasa huo na kuwaomboleza waliofariki. Pia alisema kwamba wale wote waliohusika wataadhibiwa kulingana na sheria.

Bek Air ilianzishwa 1999, ikilenga kuwabeba watu maarufu kulingana na tovuti ya kampuni hiyo.

Siku hizi kampuni hiyo inajielezea kuwa kampuni ya bei ya chini zaidi nchini Kazakhstan. Ina ndege 100 aina ya Seven Fokker. **BBC**



Polisi na wafanyakazi wa uokoaji nchini Kazakhstan, wakiendelea kutafuta watu walionusurika katika ajali ya ndege iliyotokea karibu na Uwanja wa Ndege wa Almaty jana. **PICHA: AP**

# Urusi, China, Iran zafanya zoezi la kijeshi bahari yenye utata

**MOSCOW,** Urusi

NCHI za Iran, China na Urusi zimeanza kufanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi kwenye Bahari ya Hindi na ghuba ya Oman.

Hata hivyo Urusi inasema zoezi hilo kama lisilotarajiwa la ushirikiano wa majeshi ya majini baina ya mataifa hayo.

Zoezi hilo la siku nne, lililofunguliwa katika mji wa Bandari wa Chahbahar, uliopo Kaskazini Mashariki ya ghuba ya Oman, na karibu na mpaka na Pakistan.

Ushirikiano huo una lengo la kuimarisha ulinzi katika eneo la bahari ya kanda hiyo.

Eneo la bahari linalozunguka Iran limekuwa kitovu cha mvutano wa kimataifa, kufuatia Marekani kuongeza mbinyo dhidi ya mauzo na ushafirishaji wa mafuta ya Iran.

Ofisa mmoja wa Jeshi la Majini la Iran, ameiambia televisheni ya taifa ya nchi hiyo kuwa ujumbe wa zoezi hilo ni amani, urafiki na ulinzi na ni ishara kwamba nchi hiyo haiwezi kutengwa kimataifa.

Kulingana na televisheni hiyo, luteka hiyo inajumuisha meli za uokozi na mazoezi ya kufyetua makombora.

Hapo juzi msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya China, Wu Qian, alisema mazoezi hayo ya kijeshi yataimarisha mahusiano na ushirikiano wa majeshi ya majini miongoni mwa mataifa hayo matatu.

Kwenye mazoezi hayo, China imetuma mfumo wake wa kuharibu makombora uitwao Xiningm wakati Urusi imepeleka meli tatu za kijeshi kutoka kikosi chake cha eneo la Baltiki, mzinga wa kufyetua roketi na boti ya uokozi.

Tehran imekuwa ikitafuta kuimarisha uhusiano wake wa kijeshi na Beijing na Moscow kutokana na kishindo cha vikwazo vya kiuchumi kutoka Marekani.

Luteka hiyo inaonekana kuwa jibu dhidi ya mazoezi ya kijeshi yaliyofanywa hivi karibuni na Marekani pamoja na Saudi Arabia ambaye ni mshirika wake katika kanda ya Ghuba.

Bahari ya Oman ambako luteka hiyo inafanyika ni eneo tete la majini kwa kuwa linaungana na mlango wa Bahari wa Hormuz, unaopitisha asilimia 20 ya mafuta yote yanayosafirishwa duniani.

Mnamo mwezi Mei na Juni, Marekani ilipendekeza kuweko kikosi cha jeshi la majini la nchi hiyo katika kanda hiyo ili kuzisindikiza meli za mafuta, kufutia mashambulizi dhidi ya meli kadhaa za mafuta ikiwamo za Saudi Arabia.

China na Urusi zina uhusiano wa karibu wa kidiplomasia, biashara na nishati na Iran. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

## JUMBA JEKUNDU- 33

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**



"Naona Kadili wewe umekuwa kimya tu kwa muda mrefu, mbona huchangii kitu, wakati mwenzio zimeletwa tuhuma hizi juu yake?" Mama alimuuliza Kadili.

Muda wote alikuwa ameinamia chini. Aliinua kichwa na kuwatazama wote wawili kwa zamu.

"Mama mimi nitasema kwa kifupi tu. Mimi si ndiyo mmeniteua kuwa mchumba wa Eliza?"

"Ndiyo." Mama Kadili alijibu haraka haraka.

"Na Eliza si alikwenda kwa Meze kuniulizia mimi mchumba wake mtarajiwa?"

"Sawa kabisa."

"Sasa hapo ana kosa gani?"

"Hili la kuwa na uhusiano usiofaa na rafiki yako hujalisikia?" Mama aliuliza.

Kadili alitoa kicheko cha madaha, akionekana kama mtu ambaye hajali chochote kilichotokea na kushangaza mama yake.

"Mama hakuna kitu kama hicho, namfahamu Meze na namfahamu Eliza hawawezi kufanya kitu kama hiki." Alijibu kwa kujiamini kabisa kiasi cha kuwashangaza wote wawili.

"Mama huu ni uongo na usiwe na wasiwasi. Hawa wawili kama watakuwa na uhusiano wa kimapenzi, mtu wa kwanza kufahamu nitakuwa mimi na siyo wewe mama wala mtu mwingine yoyote, kwa hiyo ulicholetewa hapa ni majungu na ndiyo maana sikutaka kuongea lolote."

Mama Kadili alichoka mwili na akili. Kwa mbali alihisi kama kuna ukweli kwenye maneno ya kijana wake.

"Haya Kadili, mimi nimekukubalia, lakini waswahili wanasema lisemwalo lipo na kama halipo laja." Alimalizia na kunyanyuka kuashiria kuvunja kikao.

"Eliza wewe nenda kapike ugali, achana na mambo haya, wala yasikunyong'onyeshe wala kukuvunja moyo, na kuona bora urudi kwenu Mtoni Mtongani, hapana.

Hapa umekuja kwa ajili yangu na utaondoka mimi nitakaposema uondoke na si mwingine. Usikasirike, haya ndiyo maisha ya mwanadamu ambayo anapitia magumu mengi, inawezekana yakawa ndiyo mwanzo wa mwanga mzuri kwetu."

Maneno ya Kadili yalimwingia kwenye mzizi wa roho Eliza. Machozi yakamtoka. Kadli akamsongelea na kumkumbatia. Akamfuta machozi kwa kutumia kitambaa.

Kila mmoja aliwaza lake. Kadili alijua kabisa kuwa Eliza hampendi, ila tu amelazimishwa uchumba kutokana na wazazi wao ambao ni mtu na dada yake kuamua hivyo kwa ajili ya kumpoza kwa machungu ya Edina.

**Unajua wanawake wanajua vitu vingi ambavyo sisi wanaume tunachukua muda mrefu sana kuvijua au kuvugundua. Na yeye ameambiwa na shoga zake, kuwa maneno mengi ambayo mama huyapata kutoka huku, basi analetewa na bibi huyo.**

Eliza naye alitambua fika kuwa ukiufungua moyo wa Kadili, utakutana na binti wa kitajiri Edina na si yeye na kama akimuoa ni kwa sababu ya shinikizo la wazazi.

Chaguo la Kadili si Eliza na wala chaguo la Eliza si Kadili.

"Usilie Eliza, tutalimaliza hili hivi karibuni, na kila mmoja wetu atakuwa na furaha tena." Alimbembeleza.

****************************

Siku mbili baadaye, Kadili alikwenda dukani kwa rafiki yake Meze. Kama kawaida alimkuta na mara nyingi humwita mtoto wa mjomba wake kukaa dukani na muda na yeye hutoka nje kuzungumza na rafiki yake.

Walikwenda kuketi kwenye gogo lililokatwa miaka mitatu iliyopita ambalo lipo chini ya mkungu, pembeni mwa duka hilo.

"Enhee niambie rafiki yangu, mbona majuzi Eliza alikuja hapa kukutafuta akasema haupo nyumbani kutwa nzima na hukuaga kabisa?" Meze alianzisha mazungumzo.

Kadili alimtazama rafiki yake na kutabasamu.

"Ahaa ndiyo siku ambayo Eliza alikuja hapa mkakumbatiana eee."

"Acha utani, nimkumbatie vipi wakati mimi niko dukani yeye yupo nje." Alijibu akijua kabisa rafiki yake anafanya mzaha.

"Nimeyapata huko nyumbani kuwa wewe na Eliza sasa hivi ni wapenzi na huwa anakuja hapa mara kwa mara usiku." Kadili alichomekea na kumfanya Meze kuangua kicheko, lakini hakikuwa halisi.

"Kwa hiyo mama yako ameambiwa hili?" Aliuliza."Siyo ameambiwa. Kulikuwa na kikao siku mbili zilizopita, mama alinita mimi na Eliza, ndiyo akaongeza maneno haya, kaambiwa na watu kuwa siku hizi unamchukua mchumba 'angu mtarajiwa Eliza."

"Hivi nani aliyekwenda kuongea maneno haya ya uongo kwenu?"

Swali hilo lilimchekesha Kadili "Hivi hadi leo bado hujamjua? Na ndiyo huyo huyo ambaye alikuwa akinasa maongezi yetu enzi zile tunakwenda disco, tukija hapa tukiongea, kesho yake mambo yote yako kwa mama."

"Nani huyo Kadili?"

"Mama Gombea." Walitazamana na kujikuta wote wawili wakiangua kicheko.

"Huyu mama jirani yangu hapa?" Aliuliza Meze.

"Sasa nani mwingine, nasikia mbea kweli, hivi tunavyoongea inawezekana kabisa akawa anatusikia."

Wakaangua tena vicheko.

"Sikiliza Kadili, ni kweli Eliza alikuja dukani hapa, lakini tulichoongea ni kwamba alikuja kununua mafuta ya kupikia, lakini pia alikuja kukuulizia kwa sababu hukuonekana kutwa nzima. Kingine nakuambia kama rafiki yangu ni kwamba alikuwa analalamika kuwa wewe ni kama unalazimishwa hivi umpende, lakini humpendi kwa dhati kwa sababu kuna mtu unampenda." Meze alimpasulia rafiki yake.

"Ndiyo ikabidi umtongoze sasa." Alichomekea, lakini kabla mwenzake hajajibu aliongeza.

"Sikiliza Meze. Ni kwamba hii habari ya kwamba mama Gombea ndiyo aliyepeleka hizi taarifa kule nyumbani, ni Eliza ndiye aliyeniambia. Unajua wanawake wanajua vitu vingi ambavyo sisi wanaume tunachukua muda mrefu sana kuvijua au kuvugundua. Na yeye ameambiwa na shoga zake, kuwa maneno mengi ambayo mama huyapata kutoka huku, basi analetewa na bibi huyo."

"Eliza yeye amekwambiaje kuhusu hili?"

"Majibu yenu yanafanana. Yeye kasema ni kweli alikuja hapa na mkaongea mambo mengi, lakini hamna uhusiano wowote ule."

"Alijibu sahihi."

"Mimi hilo halinipi tabu sana, ila nina mpango wa kumfanya Eliza awe na furaha."

"Ni kweli hana furaha, anataka uwe muwazi kwake, umchumbie kama wazazi wenu wanavyotaka au umuache awe huru." "Ni kweli Meze. Kwa nilipofikia, napenda tu kukufahamisha kuwa uwezekano wa kumuoa Eliza ni mdogo sana."

"Kwa nini?"

"Naona niko karibu mno kumpata Edina." Alijibu Kadili na macho yake yaliyonyesha kuwa ana uhakika na anachokisema.

"Umekutana naye wapi? Mumewe je itakuwaje?"

"Kwa kifupi moja ya jambo lililonifanya nije hapa ni hili. Edina alikuja hapa majuzi kunitafuta, navuka barabara tu nikaitwa na mtoto mmoja hivi, kuna gari ilikuwa imepaki, kumbe yake, alifuata tu ramani ya Tandale akanipata.

Alinichukua na kunipeleka kwenye hoteli ambayo amejificha kwa sasa. Amenihadithia vitu vingi, kumbe alioliewa kinguvu na matakwa na mama yake.

Na aliambiwa akikataa basi mama yake ataniua mimi. Akakubali. Jamaa mwenyewe kumbe ana wanawake kibao. Edina alipogundua walikorofishana akamtoroka. Mama yake Mama Pauline ndipo alipopatwa na ugonjwa na moyo na kufariki.

Hakuna hata mmoja aliyemwambia mwenzake mambo ya mapenzi, lakini vitendo vyetu na maneno vinaelekea huko.

Edina amehatarisha sana maisha yake kwa ajili yangu. Hii inaonyesha kabisa kuwa ananipenda." Kadili alijimwambafai.

**Itaendelea Jumamosi**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA COMMUNICATION CONSTRUCTION COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 805 CFU (TRUCK). Chassis namba LNJAEDA20CK804635. Engine namba B2137092.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PWA/MLA/RB/813/2019.

115568202

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M. 1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya Mwanzo KIMARA

Usimamizi wa Mirathi No. 328/2019

Ombi la SUMA ILOMO MWAKALINDILE kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu ALIPIPI ISOTE MWAKIBINGA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/01/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 24/12/2019

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIMARA
DAR ES SALAAM

115567102

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHAKIRA ATHUMANI LUKANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3439-0052 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia UMOJA Sekondari mwaka 2015.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MTW/MTW/RB/534722/2019.

115568002

## KUPOTEA KWA CHETI



**YOHANA UREMBO** amepotelewa na cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya Sekondari MINAKI, Chenye index namba S.133/100 na alimaliza mwaka 1986 na chenye rb namba PWA/CHA/RB/475543/2019.

115567702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MUSSA MAJALIWA** KISSALA anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 519 CEN. Chassis namba MD2A21BYXKWL89246. Engine namba PFZWKL10615.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/TAB/RB/579057/2019.

115567802



Post Card hii yenye mvuto na ujumbe mzito imeambatana na Chemsha Bongo. Jipatie nakala yako, kisha ujibu maswali yaliyomo. Washindi watasoma bure mafunzo ya udereva (Int Level) au Computer (Level 1).

**Kwa maelezo zaidi:**
**K-Zi 0754 663632.**
**Whatsapp +27614030842.**

115567602

## IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI
AT KINONDONI
CIVIL REVISION NO. 49 OF 2019

ELIZABETH F. MLELI……………APPLICANT
VERSUS
RANDA HOLDING LIMITED…………………..RESPONDENT

TO: RANDA HOLDING LIMITED

NOTICE OF DATE MENTION/HEARING

THE NOTICE that the above case has been fixed for Mention/Hearing on 30 day of DECEMBER, 2019 at 8:30 a.m Before Hon. J. LYIMO. YOU ARE required appearing in this Court without fail and you must Produce him on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case. Given under my Hand and the Seal of the Court this 17 Day of DECEMBER, 2019.

RESIDENT MAGISTRATE

115568102

## CHETI KIMEPOTEA



**SUNDAY ENOCK NDONONDO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye No. P0465-0263 kilichotolewa na JAMHURI SECONDARY SCHOOL mwaka 2005.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/569570/2019.

## JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **31/12/2019** kampuni ya **ESTIM CONSTRUCTION COMPANY LTD** inatarajia kusafirisha mashine (Excavator) kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea LUGOBA kutumia barabara ya MOROGORO, CHALINZE SEGERA** kupitia **VIGWAZA.** Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 235 CHW/ T 106 AYZ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20 |
| Upana | - | mita | 3.20 |
| Kimo | - | mita | 4.80 |

3. Njia itakayotumika: **MOROGORO, CHALINZE SEGERA, kupitia VIGWAZA hadi LUGOBA.**
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115568402

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Habari Motomoto**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DE LIGT ATAKA KUZEEKEA JUVENTUS



**TURIN,** Italia

BEKI Matthijs de Ligt amesema ana matumaini ya kucheza kwa muda mrefu zaidi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus.

De Ligt mwenye umri wa miaka 20, alijiunga na Juventus akitokea Ajax kwa ada ya pauni milioni 75 Julai mwaka huu, akisaini mkataba wa miaka mitano kuichezea klabu hiyo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi ana matumaini ya kubakia kwa muda mrefu hapo Turin akisema kwamba anajisikia fahari kucheza hapo Juventus.

"Nina furaha kubwa kuwa Turin, natumaini kubakia hapa kwa muda mrefu," alisema De Ligt akiiambia televisheni ya Juventus.

"Nilijisikia fahari sana kuja hapa, wakati klabu kubwa kama Juve inapokutaka ni heshima kubwa kwako.

"Mara zote nimeipenda Juve kama klabu na sasa nina furaha na najisikia fahari kuvaa jezi hii."

De Ligt ameanza katika mechi 12 za Serie A akiwa hapo Juventus, ambao kwa sasa wanalingana pointi na Inter baada ya mechi 17. Beki huyo wa kati anataka kuendelea kuimarika zaidi kwa klabu yake hiyo na ana matarajio ya kubeba taji na timu hiyo.

# *Ni ngumu kuwazuia Liverpool - Rodgers*

**LONDON,** England

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, anaamini itakuwa ni "ngumu sana, sana kuwazuia" Liverpool kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Liverpool ilijivuta kileleni kwa pointi 13 zaidi baada ya kuwafumua Leicester mabao 4-0 kwenye Uwanja wa King Power, Alhamisi.

Rodgers amesema klabu yake hiyo ya zamani, ambayo imeshinda mechi 17 kati ya 18 za Ligi Kuu msimu huu, itakuwa ni ngumu kuwazuia vinara hao.

"Wanakwenda kwa kasi sana na ni vigumu mno kuwazuia. Hakuna shaka kwamba wanajiamini na wataendelea kuwa mbele," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wamekuwa washindi na hadi sasa hawajapoteza mchezo wowote kwa kipindi cha miezi 18, hivyo kupoteza mchezo watahitaji kuwa na msimu mwingine... wamepata wachezaji wa kutosha kwa sasa na wenye uzoefu mzuri na wenye ubora.

"Bado wana mechi nyingi za kucheza, lakini mechi zetu mbili zilizopita tumekutana na timu bora zaidi kwenye Ligi Kuu."

Roberto Firmino alifunga mara mbili, huku James Milner akifunga moja kwa penalti na Trent Alexander-Arnold akafunga la nne.



# Klopp: Liverpool kuongoza sio kitu muhimu



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza kuongoza kwa Liverpool kwa tofauti ya pointi 13 kwenye ligi Kuu England "sio muhimu" baada ya kuifumua Leicester City.

Vinara hao wa Ligi Kuu England walipata ushindi mtamu pale kwenye uwanja wa King Power siku ya Alhamisi, wakishinda mabao 4-0 dhidi ya Leicester hao ambao wapo nafasi ya pili.

Roberto Firmino alifunga mawili, James Milner akafunga kwa penalti na Trent Alexander-Arnold akafunga la nne na kuwafanya Liverpool kukaa kileleni na kuongoza kwa pointi 13.

Hata hivyo, Klopp amesema kuongoza kwa pointi 13 kileleni sio muhimu sana kwa kikosi chake.

"Unachofikiria ni kile kinachobadili swali kwa tofauti ya namba: Ilikuwa 10, 11, na sasa 13," amesema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Kiukweli wala hatufikirii hilo, hatutaki kabisa kufikiria kuhusu pointi ngapi tunaongoza. Wala hatuzitaji, kwa sababu sisi tunachoangalia ni kuhakikisha tunashinda kila mchezo uliopo mbele yetu.

"Siwezi kukaa na kufikiria kiasi cha pointi tulichonacho, la msingi ni timu kucheza vizuri na kupata pointi."

**HABARI MICHEZO**

# Guardiola: Nilijaribu kumshawishi Kompany abakie

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kwamba, alijaribu kumshawishi Vincent Kompany kubakia kwa msimu mmoja zaidi hapo Manchester City.

Kompany alimaliza kipindi chake cha misimu 11 alichokaa na klabu hiyo akiwa nahodha na kuongoza kutwaa mataji matatu msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Ubelgiji alifunga bao kali la shuti kali wakati wa ushindi wa 1-0 dhidi ya Leicester City ambao ndio ulikuwa mchezaji wa mwisho wa ushindani kucheza pale Etihad, huku kikosi hicho cha Guardiola kikiwapiku Liverpool na kutwaa taji kwa tofauti ya pointi moja.

Kumekuwa na habari tofauti ndani ya klabu hiyo, kwani kwa sasa City wanakimbizwa na Liverpool.

Safu yao ya ulinzi imeyumba kutokana na kukosekana kwa Aymeric Laporte ambaye ni majeruhi na Guardiola amebainisha kwamba, kama Kompany angekuwa bado kwenye klabu hiyo angekuwa msaada, lakini kwa sasa yupo kule Anderlecht.

"Nilijaribu kumshawishi Vincent kubakia kwa mwaka mmoja zaidi na sisi," alisema kuelekea mchezo wake wa jana Ijumaa dhidi ya Wolves.






# SOLSKJAER AMLINGANISHA RASHFORD NA RONALDO

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer kwa mara nyingine tena amemlinganisha Marcus Rashford na Cristiano Ronaldo baada ya Manchester United kushinda dhidi ya Newcastle United.

Rashford alifunga bao lake la 11 kwenye Ligi Kuu msimu huu wakati United wakibuka na ushindi wa magoli 4-1 katika dimba la Old Trafford juzi Alhamisi.

Awali Solskjaer aliwahi kumlinganisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 na nyota wa zamani wa United, Ronaldo na sasa amefanya hivyo baada ya Rashford kufunga bao kali kwa kichwa.

"Ana nguvu. Anajiangalia mwenyewe na anajituma kwa bidii zaidi akiwa gym," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Ukiwa na uwezo kama ule ni jambo zuri zaidi kwa mchezaji kwani anajiweka kwenye mazingira mazuri ya kufanya lolote wakati wowote.

"Marcus anafanya kama kile anachokifanya Cristiano na anamkaribia kwa sasa maana uwezo wake ni mkubwa zaidi."

Anthony Martial alifunga mara mbili na Mason Greenwood pia alifunga kwenye mchezo huo, huku bao pekee la Newcastle, likifungwa na Matty Longstaff.

# *Xhaka akaribia kujiunga Hertha*

**LONDON,** England

GRANIT Xhaka amefikia makubaliano na Hertha Berlin na ameitaarifu Arsenal anataka kujiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo.

Majaliwa ya Xhaka pale kwenye Uwanja wa Emirates yamekuwa shakani tangu kiungo huyo alipokwaruzana na mashabiki wakati timu yake ikitoka sare ya 2-2 na Crystal Palace Oktoba mwaka huu.


Mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Monchengladbach alishika masikio yake kuwaonyesha ishara mashabiki waliokuwa wanamzomea kuwa hasikii vizuri wakati akitolewa uwanjani.

Baada ya kupokonywa unahodha na kocha wa zamani, Unai Emery, ilionekana wazi kwamba kipindi cha dirisha dogo la Januari kuna uwezekano mkubwa akaondoka.

Xhaka, ambaye alijiunga na washikabunduki hao akitokea Monchengladbach, alianza kwenye mchezo uliomalizika kwa sare ya 1-1 na Bournemouth juzi, Alhamisi ukiwa ni mchezo wake wa kwanza kwa kocha mpya, Mikel Arteta.

Hata hivyo, wakala huyo, Jose Noguera amedai kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amefikia makubaliano na Hertha inayonolewa na Jurgen Klinsmann.

"Kiukweli kabisa ni kwamba tumefikia makubaliano na Hertha na ningependa kwenda Berlin," alisema Noguera akiiambia Blick.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AJIPANGA KUMSAJILI RABIOT

●●● Mfaransa huyo anatarajiwa kuimarisha safu ya kiungo ya Arsenal...

**LONDON,** England

ILI kuimarisha safu yake ya kiungo na kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kufanya vema, Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, ameweka wazi nia yake ya kuwania saini ya kiungo wa Juventus, Adrien Rabiot.

**Kocha huyo mpya wa Arsenal amesema kuwa anataka kuona Mfaransa huyo anatua kwenye kikosi chake.**

Arteta ameanza mchakato wa kuangalia nyota mbalimbali wa kuwasajili katika dirisha dogo la Januari na amemtaja Rabiot anaweza kumsajili kwa mkopo ili kusaidia kukijenga kikosi chake baada ya kurithi mikoba ya Unai Emery, ambaye alitimuliwa klabuni hapo.

Safu ya kiungo ya Arsenal inaonekana kuyumba huku pia kukiwa na taarifa kwamba nahodha wake wa zamani Granit Xhaka anajiandaa kuondoka klabuni hapo baada ya kuingia katika mzozo na mashabiki wa timu hiyo hivi karibuni, huku Lucas Torreira na Mesut Ozil wakishindwa kuonyesha ubora wao msimu huu.

Rabiot anatajwa huenda akawa suluhisho la tatizo hilo la idara ya kiungo ya Arsenal baada ya Mfaransa huyo kukosa namba kwenye kikosi cha mabingwa hao wa Serie A msimu huu.

Juventus ilimsajili Rabiot katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana akiwa mchezaji huru akitokea PSG, lakini nyota huyo ameanza kwenye kikosi cha kwanza katika mechi tano kati ya tisa alizocheza, na Arteta anataka kumchukua kwa mkopo ili aweze kuisaidia timu yake, gazeti la The Times limeandika.

Inaelezwa kuwa, dakika alizocheza Rabiot katika mechi za Serie A msimu huu ni chache ukilinganisha na zile alizokaa langoni golikipa wa akiba wa timu hiyo, Gianluigi Buffon.

Hata hivyo, nyota huyo amekuwa akitajwa kuhusishwa na kuhamia katika Ligi Kuu England kwa muda mrefu, wakati Arsenal na wapinzani wao Tottenham wakitajwa kuonyesha nia ya kumsajili.

Akifanikiwa kutua Gunners, anaweza kuisaidia timu hiyo ambayo imekuwa na tatizo kwenye safu yake ya kiungo na inaelezwa kwamba Rabiot ana uwezo wa kucheza vema ndani ya eneo la 18, kitu ambacho kwa sasa Arsenal inakikosa.

Ujio wa Rabiot unatajwa kuisaidia Arsenal ambayo haina uhakika na hatima ya Xhaka ambaye anajiandaa kujiunga na Hertha Berlin ya Ujerumani.

## ZISIKUPITE

### XHAKA KUELEKEA UJERUMANI

WAKALA wa kiungo wa Arsenal, Granit Xhaka, amesema kuwa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Uswis ambaye ana umri wa miaka 27amekubali mchakato wa kujiunga na Hertha Berlin ya Ujerumani. ***(Blick, via Mirror)***

### DRAXLER, GUEYE SOKONI

CHELSEA imeweka wazi inahitaji kumsajili winga wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Julian Draxler (26), na kiungo wa Timu ya Taifa ya Senegal, Idrissa Gueye, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Star)***

### WILLIAN, CHELSEA WATETA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema kuwa winga wake Mbrazili Willian (31), yuko katika mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, mkataba wake wa awali unatarajia kumalizika katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### VOLLAND AWEKEWA KIGINGI

MABOSI wa Bayer Leverkusen wanajipanga kuzuia ofa yoyote kutoka Arsenal kwa ajili ya kutaka kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kevin Volland, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Mail)***

### CITY KUMBAKISHA SANE

WINGA wa Manchester City, Leroy Sane (23), ataendelea kubakia klabuni hapo mpaka mwishoni mwa msimu, lakini inaelezwa kuwa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani anatarajia kuhamia Bayern Munich kwa dau la pauni milioni 85 katika kipindi cha majira ya joto. ***(Star)***

### ELNENY ANUKIA MILAN

BABA wa kiungo wa Arsenal, Mohamed Elneny (27), amesema kuwa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Misri ambaye anaichezea Besiktas kwa mkopo, ameanza mazungumzo ya kuhamia AC Milan. ***(Express)***

### TORRES AKARIBIA CITY

MANCHESTER City inajipanga kuanza mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Villarreal Mhispania Pau Torres (22), na beki wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Dias, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### UNITED, CITY VITANI

KIUNGO wa Dinamo Zagreb na Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Olmo (21), anawindwa na klabu za Manchester City pamoja na Manchester United, huku yeye mwenyewe akisema kuwa anahitaji "kusonga mbele" katika kazi yake hiyo ya kusakata kandanda. ***(Manchester Evening News)***

### HODGSON ASAKA WATANO

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, amesema kuwa ili kikosi chake kiweze kuimarika na kukabiliana na ushindani wa Ligi Kuu England, anahitaji kusajili "wachezaji wapya wanne au watano" katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Mail)***

### HAZARD KUREJEA FEBRUARI

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Eden Hazard (28), atakuwa nje ya uwanja hadi mwishoni mwa Januari au mapema Februari, kufuatia majeraha ya enka yanayomkabili nyota huyo ambaye anaichezea pia Timu ya Taifa ya Ubelgiji. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# KOCHA AZAM AFUNGUKA KIUNGO KIMEWAANGUSHA

**Na Somoe Ng'itu**

KUKOSA umakini na idara ya kiungo kuchoka, ni sababu zilizotajwa "kuigharimu" Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

**Coastal Union ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mchezo huo na kufikisha pointi 20 sawa na Azam FC ambayo iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, huku Kagera Sugar yenye pointi 24 ikiwa ya pili na mabingwa watetezi Simba wakiwa kileleni na pointi zao 28.**

Bao hilo pekee katika mchezo huo, lilifungwa na nyota wa zamani wa Simba, Haji Ugando.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, alisema kuwa pia wachezaji wake walicheza katika kiwango cha chini katika kipindi cha pili, hali iliyowafanya wenyeji Coastal Union kutawala mchezo huo.

Cheche alisema pia hali ya uwanja wa Mkwakwani haikuwa nzuri, hivyo iliwanyima fursa wachezaji wake kucheza kandanda walilozoea.

"Umakini haukuwa mzuri, hata bao tulilofungwa lilitokana na mchezaji wangu ambaye alitoa pasi, ndio mfungaji akawahi mpira na kwenda kufunga, pia leo (juzi), tulibadilisha aina ya mfumo wa kucheza na uwanja nao haukuwa rafiki kwetu," alisema Cheche.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kuwa timu yake ilicheza kwa hatadhari baada ya kufahamu wapinzani wao wana wachezaji wenye uzoefu na ligi hiyo.

Mgunda alisema kuwa haikuwa mechi rahisi, lakini anasisitiza kwamba Ligi Kuu ni ngumu na kila timu inaingia uwanjani kusaka pointi na si kusindikiza wengine.

"Tulikuwa tunacheza na timu nzuri, timu yenye wachezaji wazuri, tuliingia kwa tahadhari, ila tunamshukuru Mungu kuwa boksi la zawadi tumelifungua, haikuwa mechi rahisi, mechi hii imekwisha, sasa tunaangalia na kujipanga kwa ajili ya mechi ijayo," alisema Mgunda.

Ligi hiyo inayatarajia kuendelea tena leo kwa vinara Simba kucheza dhidi ya KMC FC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.



Kiungo wa Simba, Hassan Dilunga (kushoto), akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Lipuli iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Jumatano iliyopita. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Wanariadha Singida mambo magumu*

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WANARIADHA watano wa Singida, waliondoka mkoani hapa jana, kuelekea jijini Mwanza kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Taifa ya mchezo huo yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo kwenye viwanja vya Butimba, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Chama cha Riadha Mkoa wa Singida, Beno Msanga, alisema kuwa idadi ya wanariadha waliokwenda katika mashindano hayo imekuwa chache kutokana na suala la ukata linalowakabili.

Msanga alisemwa kuwa, awali walitarajia kusafirisha wanariadha 15, lakini kutokana na ukosefu wa fedha walionao, imesababisha mkoa huo kuwakilishwa na wawakilishi wachache, ambao wamelazimika kujigharamia wenyewe.

Aliwataja wanariadha waliosafiri kuwa ni pamoja na Faidha Ally, Nestory Steven Hadu, Tuma Andrea, Msandai na Petro Joseph na kuongeza kuwa wanariadha wengine watano wa mkoa huo waliokuwa kambini Serengeti wataungana na wenzao Mwanza.

"Naenda kwenye mashindano ya riadha ya taifa na nakwenda kushiriki mbio za mita 5,000. Ninawaahidi wakazi wa Mkoa wa Singida na vitongoji vyake kwamba pamoja na changamoto za kiuchumi, lakini nitajitahidi mpaka nipate medali," alisema Tuma.

Hata hivyo, mwanariadha huyo alisema kuwa hali ya kutopatiwa huduma ya usafiri na maandalizi bora, inawasikitisha licha ya wao kwenda kupeperusha bendera ya mkoa.

Aliongeza kuwa wanashangazwa pia kuona viongozi wa mkoa akiwamo Ofisa Michezo ambaye alikuwa na taarifa za safari hiyo, kushindwa kujitokeza na kuwaaga wanariadha hao ambao waliamua kujisafirisha kwa gharama zao.

## Mkutano Taswa kufanyika Januari

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO Mkuu Maalum wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo nchini (Taswa), ambao awali ulipangwa kufanyika kesho Jumapili, sasa utafanyika Januari 12, mwakani.

Hatua ya kusogeza mbele mkutano huo, inatokana na maombi ya baadhi ya wanachama, ambao walichelewa kuthibitisha ushiriki wao kwa muda uliokuwa umepangwa awali, hivyo ikaonekana kuna umuhimu wa kuwapa nafasi.

Katibu Mkuu wa Taswa, Amiri Mhando, alisema jana kuwa lengo la mkutano huo ni kujadili masuala mbalimbali ya chama, ambapo pia utapokea taarifa kutoka Kamati ya Marekebisho ya Katiba iliyoundwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na pia utapokea mapendekezo kutoka Kamati ya Utendaji ya Taswa ambayo inamaliza muda wake.

Mhando alisema kuwa washiriki wa mkutano huo ni wanachama wote walioko katika leja baada ya kushiriki uchaguzi wowote wa chama hicho wa kuanzia mwaka 2004 hadi 2014, pamoja na wanachama wapya walioingia kuanzia mwaka 2015 hadi Juni mwaka huu.

Aliwataka wanachama wanaotaka kushiriki mkutano huo kuthibitisha kwa maandishi kwa kutaja jina na chombo wanachofanya kazi na kutuma kwa: taswatz@yahoo.com au mgosius@yahoo.com au machagift@gmail.com na kutaja mwisho wa kuthibitisha ushiriki ni Desemba 31 mwaka huu.

## Pawasa atamba walistahili kombe

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Ufukweni, Boniface Pawasa, amesema kuwa kikosi chake kilistahili kutwaa ubingwa wa mashindano ya Copa Dar es Salaam kutokana na kuwa na timu imara zaidi.

Pawasa alisema kuwa Tanzania iliyoanza vibaya michuano hiyo kwa kufungwa na Uganda, ilifanya maandalizi ya muda mrefu na mafanikio waliyopata, yalitokana na juhudi zao.

Beki huyo wa zamani wa Simba na APR ya Rwanda, alisema kuwa mashindano hayo yalikuwa na ushindani na kila timu iliingia uwanjani kupambana.

"Tulijiandaa kupata matokeo chanya licha ya kupoteza mchezo wa kwanza mbele ya Uganda kwa kufungwa mabao 2-1 wengi walipoteza imani kwetu na walishindwa kujitokeza kwa wingi mwisho wa siku tumefikia malengo yetu," alisema.

Mashindano hayo ambayo yanafanyika kwa msimu wa tatu, mwaka huu yalishirikisha nchi tano ambazo ni Burundi, Malawi, Uganda na Shelisheli ambayo ilipewa tuzo ya nidhamu.

# Michezo

Jumamosi Desemba 28, 2019

Nipashe



Arteta ajipanga kumsajili Rabiot HABARI UK.30



Beki wa kulia wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Newcastle, Joelinton katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi usiku. United ilishinda mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAWEKA REKODI SAMORA

## ●●● Ni baada ya kuvunja mwiko kwa Prisons msimu huu na kuwasogelea watani...

**Na Adam Fungamwango**

GOLI la dakika ya nne lililofungwa na Mnyarwanda Patrick Sibomana lilitosha kuipa Yanga pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya "Maafande" wa Tanzania Prisons iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani Iringa.

**Mechi hiyo ambayo awali ilipangwa kuchezwa Sokoine, Mbeya, lakini ilihamishwa kufuatia hali mbaya ya uwanja ya jijini humo kuharibiwa na mashabiki waliohudhuria tamasha la muziki, ilionekana kutumia zaidi nguvu kuliko ufundi.**

Yanga imevunja mwiko wa Prisons iliyokuwa timu pekee kwenye Ligi Kuu ambayo haijapoteza mechi yoyote.

Mpira wa kurushwa wa kiungo Abdul-Aziz Makame, uliwapita mabeki wa Prisons na kumkuta mfungaji aliyeukwamisha wavuni kwa mguu wa kushoto na kuwa bao lake la tatu kwenye Ligi Kuu msimu huu. Kama ingekuwa makini Yanga ilikuwa iende mapumziko ikiwa inaongoza kwa magoli matatu, kwani ilikosa mabao ya wazi yaliyotokana na mipira ya kurushwa kutoka kwa Makame.

Mshambuliaji David Molinga aliruka juu na kupiga kichwa mpira wa kurushwa, uliookolewa kwenye mstari wa goli na Laurian Mpalile na kumkuta Deus Kaseke ambaye alipaisha juu dakika ya 28, huku mabeki wa Prisons walilazimika kuokoa mara mbili kwenye mstari wa goli piga nikupige iliyotokana tena na mpira wa kurushwa na Makame dakika ya 37, huku kipa Jeremiah Kasubi, akiwa ametoka golini.

Angalau kipindi cha pili Prisons ilibadilika na kufanya mashambulizi mengi golini mwa Yanga, lakini wachezaji wake hawakuwa makini katika umaliziaji ambapo dakika ya 73 mpira ulioonekana hauna madhara, ulimpita kipa Metacha Mnata, lakini kabla haujavuka mstari wa goli aliuwahi.

Dakika ya 83, Jumanne El Fadhili, aliachia shuti kali lililotoka pembeni kidogo mwa lango la Yanga, huku dakika mbili kabla mechi kumalizika, Jeremiah Juma, aliruka juu na kupiga kichwa krosi iliyopigwa na Cleophace Mkandala, lakini ukapaa langoni na kuwa salama kwa Yanga.

Dakika za majeruhi, mchezaji wa Prisons Adili Buha alitolewa nje kwa kadi nyekundu, alipopewa kadi ya pili ya njano kwa kumchezea madhambi, Mohamed Issa.

Kwa matokeo hayo, Yanga inapanda juu kutoka nafasi ya tisa hadi ya tatu, ikiwa imefikisha pointi 21 kwa michezo 10 iliyochezwa, ikizidiwa na Simba yenye pointi 28 kwa mechi 11 na Kagera Sugar ambayo ina pointi 24 kwa michezo 13 ambayo imecheza mpaka sasa.

Prisons inakamata nafasi ya nne ikiwa na pointi 20 baada ya kushuka dimbani mara 13, huku Singida United iliyocheza pia mechi 13 ikiendelea kuburuza mkia kwa kuwa na pointi saba mkononi.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Vodacom, inatarajiwa kuendelea tena leo kwa KMC FC kuwakaribisha vinara ligi hiyo, Simba kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

## Simba, KMC majaribuni Ligi Kuu Bara

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Mwenyekiti wa zamani wa Simba, Ismail Aden Rage, akisubiri kuona timu yake inapata ushindi mnono dhidi ya watani zao Yanga hapo Januari 4, mwakani, mabingwa hao wanashuka dimbani kuvaana na KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema kuwa wamejiandaa kupambana katika mechi ya leo kwa sababu wanahitaji kuendeleza kasi ya ushindi. Nahodha na kiungo huyo wa zamani wa Simba, Matola, alisema kuwa kila mechi kwao ni sawa na fainali na wanaziheshimu timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Bara.

"Tunaendelea vizuri na maandalizi ya mechi yetu kesho (leo), dhidi ya KMC, ni mechi ngumu pia, KMC si timu mbaya, wanacheza kwa mipango na ina wachezaji wenye kasi, tutawavaa huku tukifahamu malengo yetu ni kutopoteza pointi," alisema Matola.

Naye Kaimu Kocha Mkuu wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema kuwa mechi zote za Ligi Kuu ni ngumu, hivyo wataingia uwanjani kucheza kwa tahadhari na umakini zaidi.

"Ligi Kuu ni ngumu, ila tumejipanga kuingia tofauti katika mechi ya kesho (leo), dhidi ya Simba, hii ni kutokana na wapinzani wetu kubadilika, tunaamini tukicheza kwa utulivu, hatutapoteza mchezo," alisema kocha huyo ambaye amerithi mikoba iliyoachwa na Mganda Jackson Mayanja.

Simba itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0 walioupata katika mechi iliyopita dhidi ya Lipuli FC kutoka Iringa, wakati KMC FC wao wakiwa ugenini walichapwa mabao 2-1 na Polisi Tanzania. Rage amesema kuwa anakiamini kikosi chake na ubora umeongezeka kufuatia marekebisho yaliyofanywa katika benchi la ufundi.

"Yanga wakipata bahati siku ile ya tarehe 4, itakuwa ni mabao 7-0, kwa hali ya sasa nilivyoiona, na hali ya Yanga ilivyo, itawachukua karne moja kuifunga Simba, mechi ya Jumamosi ni kayaya kaka," alisema Katibu Mkuu huyo wa zamani wa Chama cha Soka Tanzania (FAT sasa TFF).

Aliongeza kuwa watani zao Yanga wameshakata tamaa, na anaamini kama mipango itakwenda vema, Simba itaonyesha kandanda la kiwango cha juu.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 28 baada ya kucheza mechi 11 wakati Singida United yenye pointi saba na imeshuka dimbani mara 13 inaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >